# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 017 ISSN 1821 - 8253 SEPTEMBA - OKTOBA 2014



## Kasi ya ukuaji wa sekta ya Afya Zanzibar yaongezeka

- Madaktari 38 kwa pamoja wahitimu Chuo cha Madaktari cha Zanzibar

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Ali S. Hafidh

**Waandishi**
Said J.Ameir
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed


## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.


Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.



P.O.BOX: 2422

Zanzibar - Tanzania

Phone: +255 223 081/5

Fax: 024 223 3722

Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz


# Maoni ya Mhariri

## Wananchi waarifiwe mafanikio, changamoto za Serikali yao

Ifikapo Novemba 3, 2014, wananchi wa Zanzibar watatimiza miaka minne (4) tokea waliposhuhudia kuapishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, ambaye ni Rais wa kwanza wa Zanzibar kuunda na kuongoza Serikali ya kwanza ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Hii ni historia katika maendeleo ya kisiasa Zanzibar na itaendelea kusomwa na vizazi vya sasa na vijavyo hasa inapozingatiwa mazingira halisi ya kisiasa yaliyokuwepo kabla, na hatimaye kupelekea kuundwa kwa Serikali hiyo.

Kimsingi, tukio la kuanzishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa lilionekana kuwa ni la lazima miongoni mwa wananchi wa Zanzibar, kutokana na uhasama mkubwa wa kisiasa uliokuwepo wakati huo baina ya vyama vikuu vya siasa Zanzibar - Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho ndicho Chama Tawala na Chama cha Wananchi CUF, ambacho ndicho chama kikuu cha upinzani Zanzibar.

Tofauti za kisiasa baina ya vyama hivyo zilidumu kwa takriban miaka 15 baada ya kuanza uchaguzi mkuu wa kwanza uliovishirikisha vyama vingi vya siasa. Katika uchaguzi mkuu wa kwanza mwaka 1995 Chama tawala kilikishinda Chama kikuu cha upinzani, lakini chama hicho cha upinzani kiliyakataa matokeo ya uchaguzi huo na vile vile kilikataa kuitambua Serikali ya wakati huo, iliyokuwa ikiongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Salmin Amour Juma.

Uchaguzi mwengine wa mwaka 2000 na mwaka 2005 pia mgombea wa CCM Dk. Amani Abeid Karume alishinda. Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa mwaka 1995, Chama kikuu cha upinzani vile vile kiliyakataa matokeo ya chaguzi hizo na katika kipindi cha karibu miaka minane katika miaka kumi aliyoongoza Dk. Amani Abeid Karume, chama hicho hakikuitambua Serikali iliyokuwa ikiongozwa na Dk. Amani Karume. CUF kilianza kuitambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi cha miaka miwili ya mwisho ya uongozi wa Dk. Amani Abeid Karume, baada ya kuanza mchakato wa mazungumzo kuhusu mabadiliko ya katiba ya Zanzibar baina ya Rais wa wakati huo Dk. Amani Abeid Karume ambaye alikuwa pia Makamo Mwenyekiti wa CCM na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad. Mazungumzo hayo yalikuwa na lengo la kuunda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Hatua ya Chama hicho cha upinzani ya kutoitambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa zaidi ya miaka kumi, ilikuwa na athari mbaya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Zipo baadhi ya nchi ambazo zilikatisha misaada yake kwa Zanzibar kutokana na kile kilichokuwa kikidaiwa kuwa ukiukwaji wa haki za binadamu. Uhasama wa kisiasa ulikua na kufikia kiasi cha kutishia amani ya nchi, uchumi wa nchi ulidorora, watoto wachanga walinyimwa chanjo muhimu, baadhi ya wakati Serikali ilishindwa kulipa mishahara ya watumishi wa umma kwa wakati na baadhi ya familia zilifarikiana kwa sababu za kisiasa.

Uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 ambao Dk. Ali Mohamed Shein alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ndio uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi ambao, CUF kimeyakubali matokeo yake na hivyo kuitambua rasmi Serikali iliyoundwa kwa mujibu wa mabadiliko ya kumi ya Katiba ya Zanzibar.

Kuanza kwa mfumo huo ndipo hasa historia ya kisiasa Zanzibar inapoendelea kuchukua nafasi yake. Wataalamu wengi na wafuatiliaji wa masuala ya kisiasa za Zanzibar hawakuwa na matumaini makubwa na muundo huo mpya wa Serikali na waliamini kwamba mfumo huo kamwe usingeweza kuiondoa Zanzibar kwenye mifarakano ambayo ilianza kuonekana kama kwamba ndio siasa za visiwa hivi.

Katika mikutano yake tofauti ya kampeni pamoja na mikutano na wadau mbali mbali kabla ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliahidi kuisimamia kwa umakini mkubwa katiba ya Zanzibar, kudumisha amani na utulivu kama ilivyokuwa imeelezwa ndani ya katiba na ndani ya Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015.

Akizungumza na waandishi wa habari mara tu alipowasili nchini kutoka ziara ya kikazi nchini Comoro hivi karibuni, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliwataka waandishi wa habari nchini kuzungumzia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne tokea kuanzishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa, badala ya kuandika taarifa ambazo hazina tija kubwa kwa maendeleo ya taifa.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa imefanya kazi kubwa katika kipindi kifupi, na kwamba mataifa mbali mbali ya Bara la Afrika na nje ya Bara hili, yamekuwa yakiitembelea Zanzibar kujifunza namna ya kuendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mafanikio.

Aidha, alisema washirika mbali mbali wa maendeleo wamekuwa wakielezea kufurahishwa kwao na namna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyotekeleza miradi yake ya maendeleo ambayo inaendeshwa kwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo, akitoa mfano hai wa ujenzi wa Skuli 21 za Sekondari Unguja na Pemba ambao umefanyika ndani ya kipindi cha miaka mitatu badala ya miaka mitano iliyokuwa imepangwa.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi zawadi maalum Salama Makame Pandu akiwa ni miongoni mwa wanafunzi bora katika Mahfali ya Kwanza ya Chuo cha Madaktari Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Mbweni nje ya Mji wa Unguja, Septemba 28, 2014 katikati ni Dk. Salhiya Ali Muhsin Mkurugenzi Idara ya Tiba.*

# Kasi ya ukuaji wa sekta ya Afya Zanzibar yaongezeka

## ■ Madaktari 38 kwa pamoja wahitimu Chuo cha Madaktari cha Zanzibar

Jumapili ya tarehe 28 Septemba 2014, itabakia kuwa siku ya kumbukumbu miongoni mwa wananchi wa Zanzibar, ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi kwenye sherehe za aina yake za mahafali ya kwanza ya Chuo cha Madaktari cha Zanzibar – "Zanzibar Medical School" yaliyofanyika katika Chuo cha Afya kilichopo Mbweni.

Mahafali hayo ni kielelezo thabiti cha mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada zake za kukuza elimu na huduma za afya nchini na ni ushahidi wa kutosha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitekeleza kwa vitendo azma yake ya kuwapatia wananchi wake huduma bora za afya.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitoa umuhimu wa aina yake kwenye sekta hii kutokana na ukweli kwamba sekta ya afya ina umuhimu wa pekee katika jitihada za kuimarisha na kudumisha hali ya afya za wananchi na ustawi wao, na kwamba Serikali haitoweza kufanikisha malengo yake ya kuwaletea maendeleo wananchi wake bila ya wananchi hao kuwa na afya njema.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa historia ya uimarishaji wa sekta ya afya katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni ya muda mrefu. Wakati wa kupigania uhuru kwenye kampeni za uchaguzi wa mwisho uliofanyika tarehe 8 Julai, 1963 kati ya mambo muhimu ambayo Chama cha ASP kiliyaahidi kuyafanya, ni pamoja na kuimarisha huduma za afya ikiwa ni pamoja na kutoa huduma za matibabu bure kitakapoingia madarakani.

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kutekeleza kwa vitendo ahadi zote zilizotolewa na Afro-Shirazi Party na baadae CCM kuhusu sekta ya afya. Maendeleo makubwa yaliyopatikana katika sekta ya afya yalielezwa kwa kina na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika hotuba yake aliyoitoa kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kiwanja Amaan mjini Zanzibar tarehe 12 Januari 2014.

Imebainika wazi kwamba tokea Mapinduzi ya Januari 1964, juhudi maalum zimekuwa zikichukuliwa na Serikali za kupatikana madaktari wa kutosha, kuongeza wafanyakazi wapya wa afya, kuwapa dhamana za kazi muhimu na kuwaandalia mafunzo kwa ajili ya kuendeleza kazi zao.



*Miongoni mwa wahitimu wa Mafunzo ya Udaktari wapatao 38 wakila kiapo cha Utii wa kazi zao mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika mahfali ya kwanza yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Mbweni nje ya Mji wa Unguja,, tarehe 28 Septemba, 2014*

Hata hivyo, pamoja na juhudi zote zilizochukuliwa, tatizo la upungufu wa madaktari limeendelea kuwepo na Serikali imekuwa ikiendelea kulitafutia ufumbuzi kidogo kidogo.

Kuanzishwa kwa "Zanzibar Medical School" kwa utaratibu maalum mnamo mwaka 2007 ikiwa na wanafunzi 40, kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha Matanzas cha Cuba, ni miongoni mwa jitihada za Serikali kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo sugu la madaktari hapa Zanzibar. Mwaka mmoja baadae, wanafunzi wawili wa udaktari waliacha masomo yao na chuo kilibakia na wanafunzi 38 waliohitimu kwenye mahafali hayo. Kadhalika, mnamo mwaka 2009 chuo kilipokea wanafunzi wengine 12 ambao wanakaribia kumaliza mafunzo yao. Tangu kilipoanza hadi sasa, Chuo hicho kinaendeshwa kwa mafanikio makubwa na Wizara ya Afya ya Zanzibar.

Ingawa mafanikio mengine vile vile yamekuwa yakiripotiwa kwenye sekta ya afya, tukio la kuhitimu madaktari 38 kwa wakati mmoja linaonekana kuwa ni tukio kubwa la aina yake. Hayo ni mafanikio makubwa siyo tu kwa kuwa Serikali imeweza kutoa idadi kubwa ya madaktari kwa wakati mmoja, lakini vile vile kwa kuweza kutoa idadi kubwa ya madaktari waliopata mafunzo yao hapa hapa nchini kupitia Chuo cha Madaktari cha Zanzibar kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Matanzas cha nchini Cuba.

Tukio hilo limewathibitishia baadhi ya watu waliokuwa na wasi wasi kwamba kuanzishwa mafunzo hayo hapa Zanzibar kusingelileta tija yoyote kwa Serikali na wananchi, kutokana na kile walichokuwa wakidai kwamba, kulikuwa hakuna maandalizi ya kutosha na pia kulikuwa hakuna utaalamu na nyenzo katika kuyaendesha mafunzo hayo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba madaktari wote wa Zanzibar wakiwemo vijana waliohitimu wanapata fursa za kujiendeleza na kuwa madaktari bingwa katika nyanja mbali mbali.

"Tutaandaa programu maalum ambayo itawapa nafasi madaktari wetu hawa wapya kusomea fani ya ubingwa ile ambayo Serikali yetu tunaihitaji kwa mujibu wa mipango yetu na ile ambayo daktari mwenyewe atakuwa tayari kuisomea. Tutatoa kipaumbele kwa zile fani zenye mahitaji makubwa", alisema Dk. Shein.

Juhudi nyengine zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na kuimarisha mashirikiano mazuri inayopata kutoka kwa wananchi na washirika wa maendeleo. Juhudi hizo zimeiwezesha Serikali kupata mafanikio makubwa katika kuimarisha huduma za afya mwelekeo ukiwa kufikia lengo lililowekwa la kuwa daktari mmoja



awahudumie wananchi 6,000, ambalo bado halijafikiwa.

Takwimu zinaonesha kuwa uwiano wa daktari kwa idadi ya watu umekuwa ukiimarika kwa kadri nchi inavyoendelea. Katika mwaka 1992 uwiano ulikuwa daktari mmoja kwa wananchi 58,000. Hadi mwezi Januari mwaka huu, wakati Zanzibar inaadhimisha Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, uwiano wa daktari kwa idadi ya watu ulikuwa ni daktari mmoja kwa wananchi 18,982.

Ni dhahiri kuwa uwiano huo utakuwa bora zaidi katika kipindi kifupi kijacho, hasa baada ya Serikali kuwaajiri madaktari hao wapya na watakaporejea masomoni vijana wengine wengi waliopo Tanzania Bara, China, Urusi, Ukraine na kadhalika.

Vile vile Serikali ina matarajio makubwa ya kupunguza idadi ya watu wanaohudumiwa na daktari watakapomaliza mafunzo yao wanafunzi waliojiunga mwaka jana katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Iko kila ishara kuwa katika miaka michache ijayo Serikali itaweza kufikia uwiano unaopendekezwa na Shirika la Afya Duniani wa angalau watu elfu kumi (10,000) kwa daktari mmoja kwa nchi zinazoendelea.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa yaliyorikodiwa, zipo changamoto mbali mbali zinazowakabili madaktari katika kutekeleza majukumu yao ya kuwatumikia wananchi. Miongoni mwa changamto hizo ambazo Serikali imekuwa ikizifanyia kazi ni pamoja na uhaba wa madaktari, wataalamu katika sekta ya afya, vifaa na nyenzo mbali mbali. Kadhalika changamoto nyengine ni kutokuwa na kitivo cha tiba cha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar ambacho kingeweza kuwasajili wanafunzi wengi zaidi kwa wakati mmoja.

Katika kulishughulikia tatizo la kutokuwa na kitivo cha utibabu (Faculty of Medicine/School of Medicine), mwezi wa Mei, mwaka 2012 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuanzisha Skuli ya Sayansi za Afya na Tiba katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Huu ni uamuzi wa msingi ambapo Zanzibar imepata uwezo wa kufundisha madaktari watakaotambulikana kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Utaratibu huu utaihakikishia Serikali kwamba mafunzo ya udaktari yanafundishwa kila mwaka na yanakuwa endelevu. Chini ya utaratibu huo, Serikali itaweza kupanga yenyewe mahitaji yake halisi ya madaktari wanaohitajika kila mwaka, kwa kila Idara na kwa kila fani. Ni dhahiri hatua hii itazidi kuleta maendeleo makubwa katika sekta ya afya.

Kadhalika, utaratibu wa aina hii utaweza kuwashajihisha madaktari kusomea fani ambazo kwa sasa hazina wataalamu wa kutosha na kwa sababu moja au nyengine, zimekuwa zikikwepwa kama vile "Pathology, Histopathology, Chemical Pathology (Clinical Biochemistry), Haematology, Microbiology, Immonology, Forensic Medicine, Paediatrics and Child health, Oncology na Psychiatry". Fani hizi ni muhimu na zinahitajika sana katika jamii.



*Mkuu wa Kitivo cha Tiba DEAN Ulpiano Perez kutoka Cuba akimtunuku Shahada Wardat Rashid akiwa ni miongoni mwa wanafunzi 38 waliohitimu mafunzo ya Udaktari katika Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya wakati wa mahfali ya kwanza yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo Mbweni nje ya Mji wa Unguja, tarehe 28 Septemba, 2014*

Vile vile, hatua ya ufundishaji wa madaktari na wataalamu wa afya katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) utawezesha kuwafundisha madaktari na wataalamu wengine wa afya wengi kwa wakati mmoja na kwa muda mfupi zaidi ikilinganishwa na utaratibu wa hivi sasa wa kufundisha mabingwa hao mmoja mmoja katika vyuo tofauti. Hilo litawezekana kwa vile madaktari wengi watakuwa wakihitimu mafunzo yao kwa wakati mmoja.

Katika hatua nyengine ya kukiimarisha Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya, chuo hicho nacho kiliunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Lengo la Serikali ni kuongeza ufanisi na kuandaa wataalamu wa fani za afya katika kiwango cha shahada mbali mbali. Utaratibu huu uliotumika kwa Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya pia umetumika kukiunganisha Chuo cha Utalii cha Maruhubi na Chuo cha Utawala wa Fedha cha Chwaka. Vyote hivyo vitakuwa chini ya Chuo Kikuu cha SUZA.

Kwa upande wa Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya, ni jambo la faraja kwa uongozi wa chuo hicho pamoja na wanachuo kwa jumla kwa vile kuunganishwa kwao na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kutawapa fursa wahitimu kupata shahada/digrii zao kupitia chuo kinachotambulikana Kitaifa na Kimataifa.

Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo inaendelea kuimarisha hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kuifanyia upanuzi kwa kuongeza baadhi ya majengo, ili iweze kutoa huduma katika kiwango cha Hospitali ya Rufaa.

Vile vile, Hospitali ya Abadalla Mzee ya Pemba inajengwa upya na kupatiwa vifaa vipya vya kisasa. Aidha, juhudi za kuzipandisha daraja Hospitali za "Cottage" za Makunduchi na Kivunge zimefikia hatua kubwa na kwa upande wa Micheweni na Vitongoji hatua zinaendelea. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikishajihisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta ya afya jambo ambalo limekuwa likisaidia sana katika kuimarisha huduma za afya nchini.

Katika jitihada za kuimarisha maslahi na ustawi wa wafanyakazi, Serikali inaendelea kurekebisha Miundo ya Utumishi (Scheme of service) ya wafanyakazi wa sekta ya afya wakiwemo madaktari kwa lengo la kuhakikisha kuwa maslahi yao yanaongezeka ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kwa bidii zaidi.

Rais wa Zanzibar aliwataka wahitimu hao na wafanyakazi wote katika sekta ya afya kuendelea kufanya kazi zao kwa uzalendo na kwa moyo mmoja na kwa kuzingatia maadili ya kazi yao, kama madaktari walivyokula kiapo chao kwenye sherehe hizo. Alisisitiza haja ya kuendelea kuwa na mapenzi na imani kubwa kwa nchi yao, huku akiwataka kujiepusha na dhana ya kwamba kufanya kazi nje ya nchi yao ndio njia rahisi ya kujipatia maslahi bora zaidi.

"Hamna budi kukumbuka usemi usemao "Mtu kwao ndio ngao". Ni lazima mzingatie kuwa Serikali imegharamika sana kukufikisheni hapo mlipo. Hivi sasa Serikali, wananchi na wazazi wenu wana matumaini makubwa ya kupata huduma zenu kama ni matunda ya jitihada na nyenzo walizokuwa wakiwekeza kwa kipindi chote cha masomo yenu haya na kabla ya haya" aliongeza Dk. Shein.

"Nasaha zangu kwenu ni kufanya kazi kwa bidii, nidhamu na kushikamana na maadili ya kazi yenu. Nataka muwe tayari kwenda kufanya kazi popote pale mtakapopangiwa na Serikali kwa kuzingatia sheria ya Utumishi wa Umma, kwani huduma zenu zinahitajika sehemu zote, mijini na vijijini, Unguja na Pemba" alisema.

Alisema udaktari ni kazi kubwa ambayo inahitaji nidhamu ya hali ya juu katika kuwahudumia wagonjwa na wananchi wote kwa jumla. Kwa hivyo, ni lazima kila wakati wawe wanakumbuka kuwa wapole, lakini wakakamavu kwenye kazi na huku wakionesha mapenzi makubwa kwa wagonjwa wao.

# Ushirikiano ndio suluhu ya changamoto ya nchi za visiwa vidogo



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akitoa hutuba yake katika Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Nchi za Visiwa Uliofanyika Apia nchini Samoa akimuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 01 Sept 2014*

Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Nchi za Visiwa Vidogo Zinazoendelea (SIDS) uliofanyika hivi karibuni katika visiwa vya Samoa, umebaini kuwa ushirikiano wa dhati miongoni mwa mataifa hayo ndiyo njia pekee rahisi itakayoweza kusaidia kukabiliana na changamoto ndani ya nchi hizo na kupata maendeleo endelevu.

Mkutano huu ni mmoja miongoni mwa mikutano iliyofuatiliwa kwa karibu na mabilioni ya watu duniani kote, hasa watu wa nchi za visiwa zinazoendelea. Takriban washiriki 3,500 kutoka nchi, Mashirika ya Kimataifa na taasisi binafsi pamoja na vyombo vya habari walikutana mjini Apia kwa siku nne kuanzia tarehe 1 hadi 4 Septemba, 2014 kujadili masuala muhimu yanayohusu maendeleo endelevu katika nchi hizo.

Takriban wawakilishi wa zaidi ya nchi 180 na mashirika mbalimbali walipata nafasi ya kuwasilisha hotuba zao katika kipindi cha siku 4, miongoni mwao walikuwepo viongozi na wakuu wa Serikali 22, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa mmoja wao.



*Washiriki wa Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Nchi za Visiwa kutoka Nchi mbali mbali Duniani uliofanyika Nchini Samoa wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akitoa hutuba yake alipomuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 01 Septemba 2014*

Licha ya kuwasilisha hotuba yake katika mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vile vile ilipata fursa kushiriki katika mijadala mbalimbali iliyokuwa ikiendelea sambamba na mkutano huo.

Nchi za SIDS ni nchi zenye mazingira yanayofanana ambayo yanaelezwa kuwa kikwazo katika kufikia maendeleo endelevu. Mazingira hayo ni pamoja na kuwa nchi ndogondogo, kuwa mbali na kutofikika kwa urahisi, kukabiliwa na majanga ya asili mara kwa mara.

Mambo haya pamoja na sababu nyingine zilizo nje ya uwezo wao, ni miongoni mwa mambo yanayodaiwa kuifanya safari ya nchi hizo kufikia maendeleo endelevu kuwa ya mashaka ikilinganishwa na nchi nyingine katika kundi la nchi zinazoendelea.

Kwa hivyo, mkutano huo ulikuwa ni fursa ya kipekee kwa nchi hizo na washirika wa maendeleo kujadili na kupendekeza namna ya kukabiliana na changamoto zinazozikabili nchi za

visiwa zinazoendelea katika kutekeleza azma yake ya kupata maendeleo endelevu.

Katika hotuba ya msingi kwenye mkutano huo iliyotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitumia fursa hiyo kueleza msimamo wake kuhusu mkutano huo ambao kaulimbiu yake ilikuwa ni Maendeleo Endelevu katika Nchi Ndogo za Visiwa Zinazoendelea kwa ushirikiano Thabiti na Endelevu.

Mbali ya kuwahakikishia wajumbe kuwa inaunga mkono kwa dhati maudhui ya mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisisitiza haja ya mataifa duniani kuimarisha ushirikiano na kuongeza nguvu ili kuziwezesha nchi zinazoendelea zikiwewo za visiwa kukabiliana na ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kwa hivyo, rai ya Tanzania kwa nchi washiriki wa mkutano ule ilikuwa ni kuzitaka nchi zinazoendelea kwa umoja wao kuzishawishi nchi zilizoendelea kuongeza uhaulishaji wa teknolojia salama zisizochafua mazingira, kusaidia kuzijengea uwezo na kuhakikisha kunakuwepo fedha zaidi kuziwezesha nchi hizo kukabialiana na majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

Sambamba na hilo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliona kuwa suala jingine muhimu la kuzingatiwa ni ushirikiano katika kuanzisha ajenda za maendeleo baada ya mwaka 2015 ambapo, kwa maoni yake katika masuala ya kupewa kipaumbele mojawapo liwe ni la kuongeza kasi katika jitihada za uhifadhi wa mazingira ili kukabiliana na athari za mazingira zikiwemo za mabadiliko ya tabianchi.

Msimamo huo unatokana na ukweli kuwa, suala la mabadiliko ya tabianchi ndio tishio kubwa la uhai na uwepo wa nchi za visiwa, na kuwa huo ndio ukweli wa maisha ya kila siku ya wananchi wa nchi hizo ambao wanashuhudia athari za mabadiliko hayo katika shughuli zao za maisha ya kila siku kama vile katika




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa na baadhi ya ujumbe aliofuatana nao akiangalia vitu mbali mbali alipotembelea Makumbusho ya Taifa Nchini Samoa katika ziara ya Kiserikali alipohudhuria katika Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Nchi za Visiwa, tarehe 01 Septemba 2014*

shughuli zao za uvuvi, kilimo na hata katika huduma za maji.

Halikadhalika pamoja na kipaumbele cha kukabiliana na athari za tabianchi kuzingatiwa, Tanzania iliikumbusha pia Jumuiya ya Kimataifa umuhimu wa kuyapa nafasi ya mbele katika ajenda ya maendeleo baada ya mwaka 2015 malengo ya Milenia ambayo bado hayajafikiwa.

Kwa kuwa suala la maendeleo linahitaji ushirikiano wa washirika mbalimbali, na kwa kuwa maendeleo yenyewe yanahusu nchi masikini na kwa kuangalia mazingira halisi kuhusu tatizo la mabadiliko ya tabianchi, ushirikiano miongoni mwa washirika mbalimbali lilikuwa miongoni mwa masuala ya msingi yaliyojadiliwa katika mkutano huo.

Hivyo mbali ya wasemaji kutoka nchi na mashirika mbalimbali kulitilia makazo wakati wa kutoa taarifa zao rasmi lakini suala hilo lilizungumzwa kwa kina katika midahalo mbalimbali iliyokuwa ikiendeshwa wakati wa mkutano huo, ambayo ilikuwa imegawanyika katika mada mbalimbali. Miongoni mwa mada hizo ni Maendeleo Endelevu ya Kiuchumi, Mabadiliko ya Tabianchi na kujikinga na Maafa, Nishati Endelevu, Maendeleo ya Jamii, Afya, Vijana na Wanawake; Bahari na Bioanuai; maji, upatikanaji wa chakula na usimamizi wa taka.

Midahalo hiyo ilikuwa na nia ya kubadilishana uzoefu kuhusu jinsi ya kufanya ubia na mashirikiano katika kukabiliana na changamoto zinazozikumba Nchi Ndogo za Visiwa Zinazoendelea na jinsi ya kutumia fursa walizonazo katika kujiletea maendeleo.

Hivyo midahalo hiyo ilibainisha kuwa misingi ya kuwa na ushirikiano na ubia katika kukabiliana na changamoto ndio bora zaidi kwa nchi hizo kuliko kutegemea misaada kutoka mashirika na nchi zilizoendelea kama uzoefu unavyoonesha.

Ni kweli usiofichika kuwa pamoja na changamoto zilizopo, Nchi za Visiwa Vidogo Zinazoendelea zina fursa nyingi za kufanya ubia na kujiletea maendeleo kupitia utalii; uvuvi, nishati endelevu, rasilimali za madini, mafuta na gesi; na ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo.

Ilielezwa vile vile katika mdahalo huo kuwa, mchango wa aina yoyote uwe wa kuzijengea uwezo nchi hizo kifedha, kiufundi, ubadilishanaji wa uzoefu au upatikanaji wa tekinolojia sahihi kwa mazingira ya nchi za visiwa zinazoendelea, utakuwa na umuhimu wa kipekee na thamani kubwa kwa

maendeleo na haunabudi kukaribishwa kwa mikono miwili.

Sambamba na hilo suala jingine muhimu ni kuwepo kwa dhamira ya kweli ya washirika katika ushirikiano huo kwa kuwa tayari na huru kupeana taarifa na kubadilishana uzoefu ili mafunzo yanayopatikana yaweze kuzisaidia nchi hizo ama kwa kuiga maendeleo yaliyofikiwa au kuepuka kurudia makosa.

Katika mnasaba huo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwaeleza washirika wa mjadala huo kuwa inatambua fika kuwa mabadiliko ya tabianchi ni moja ya changamoto kubwa inayohatarisha sio tu nchi za visiwa, lakini pia ulimwengu wote kwa hivyo juhudi za pamoja hazina budi kufanyika kukabiliana na mabadiliko hayo.

Kwa hivyo ilipongeza majadiliano hayo kuhusu ushirikiano kati ya nchi za visiwa na wadau kwa kuwa yamekuja kipindi muhimu cha jitihada za dunia za kuziba pengo na kuonesha mwitikio wa kimataifa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kuhakikisha mustakbala wa baadae wa nchi za visiwa.

Moja miongoni mwa ishara za mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mkutano huu ni kwa washiriki kwa kauli moja kupitisha waraka wenye vipengele 124. Waraka huo, pamoja na mambo mengine umeainisha mikakati ya kuzikwamua nchi hizo kwenye kuimarisha sekta ya Utalii; masuala ya mabadiliko ya tabianchi; Usalama wa Chakula na Nishati endelevu.

Aidha, azimio hilo limetaja namna ya utekelezaji wa mipango na malengo ya nchi za visiwa, kama yalivyobainishwa katika mkutano wa kwanza wa SIDS uliofanyika nchini Barbados mwaka 1994, mkutano wa pili uliofanyika nchini Mauritius mwaka 2005 na matokeo ya mikutano mingine mbalimbali ya kimataifa.

Matarajio ya washiriki wa mkutano huo ni kuwa waraka huo utakuwa ni sauti na mkakati wa nchi za Visiwa Vidogo Zinazoendelea katika majadiliano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo majadiliano ya ajenda mpya za maendeleo baada ya mwaka 2015 na mikutano mbalimbali ya kimataifa kuhusu mabadiliko tabianchi.

Miongoni mwao, ni Mkutano wa Mabadiliko ya Tabia Nchi uliofanyika mwezi Septemba 2014 huko New York; Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi utakaofanyika Lima, Peru mwezi Desemba 2014; Mkutano wa Tatu wa Kukabiliana na Majanga, utakaofanyika Miagi, Japan mwezi Machi 2015; na Mkutano wa nne wa Uwezeshaji Kifedha kwa Ajili ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo, utakaofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Juni 2015.

# Zanzibar na Muungano wa Comoro zimefungua ukurasa mpya wa ushirikiano

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara rasmi ya kiserikali katika Muungano wa Comoro, ziara ambayo imezifanya nchi hizo mbili za visiwa kufungua ukurasa mpya wa mashirikiano katika sekta mbali mbali. Katika makala haya, Jarida la Ikulu linaelezea namna ziara hiyo ilivyofungua ukurasa huo mpya wa ushirikiano kati ya Zanzibar na nchi hiyo.

Wananchi wa Zanzibar na Comoro wamekuwa na mahusiano ya karne



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Muungano wa Comoro Mhe, Mohamed Ali Soilihi wakiwapungia mikono wananchi waliohudhuria katika mapokezi yake katika uwanja wa Ndege wa Nchini Comoro katika ziara kwa mualiko wa Rais wa Comoro Dk Ikililou Dhoinine, tarehe 15 Septemba 2014*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Muungano wa Comoro Mhe. Mohamed Ali Soilihi wakipokea heshima ya utii pamoja na kupigiwa nyimbo za Mataifa yao katika uwanja wa ndege wa nchini Comoro wakati wa mapokezi ya ziara kwa mualiko wa Rais wa Comoro Dk. Ikililou Dhoinine, tarehe 15 Septemba 2014*

nyingi na kwa miaka mingi wamekuwa wakitembeleana kwa usafiri wa bahari uliokuwa ukitegemea pepo za Kusi na Kaskazi, ambapo majahazi yalikuwa yakisafiri kati ya bandari ya Malindi, Unguja na ile ya Mitsamihouli katika kisiwa cha Ngazija.

Mahusiano hayo yamewafanya wananchi wa nchi hizo kuwa na utamaduni, mila na desturi zinazofanana ikiwemo vyakula, mavazi na hata dini. Mahusiano hayo yalitoa fursa kwa watu kuchagua sehemu za kuishi na kuamua ama kuishi Zanzibar au Comoro na hivyo kuyafanya mahusiano ya watu wa sehemu hizo kuwa ya damu.

Uhusiano kati ya wananchi wa Zanzibar na Comoro hauishii tu katika ngazi ya jamii lakini hata katika ngazi rasmi za kiserikali. Kutokana na sababu hiyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alifanya ziara rasmi ya kiserikali nchini humo.

Kwa hakika ziara hiyo lengo lake kuu lilikuwa, kwa upande mmoja, kuimarisha uhusiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Muungano wa Comoro na kwa upande wa pili, kuimarisha ushirikiano kati ya Zanzibar na nchi hiyo.

Akiwa nchini Comoro, Mheshimiwa Rais alipata fursa ya kufanya mazungumzo rasmi na Rais wa nchi hiyo Dk. Dhonine Ikililou, alikutana pia na Makamu wa Rais wa nchi hiyo Mheshimiwa Ali Mohamed Soilihi pamoja na Gavana wa Ngazija Mheshimiwa Moingibaraka Said Soilihi.

Vile vile Dk. Shein alitembelea sehemu mbalimbali za Comoro ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Comoro, Kitivo cha Dini na Lugha ya Kiarabu, kiwanda cha kutengeneza boti za uvuvi, kiwanda cha kusindika mafuta ya maua ya mlangilangi, vanilla na ghala la karafuu pamoja na sehemu za kidini.

Aidha, alitembelea maeneo yenye kumbukumbu za kihistoria zenye kuonesha fungamano la watu wa Zanzibar na Comoro kidini na kijamii ikiwemo Mji wa Mitsamihouli.

Maeneo haya aliyopangiwa na wenyeji wake yalilenga katika kubadilishana uzoefu katika masuala yanayofanana kila upande ili kuona namna gani nchi hizo zingeweza kusaidiana na pia kukumbushana kistoria ya ushikiriano wa watu wa nchi mbili hizo.

Ni jambo la kujivunia kuwa ziara hiyo imetoa matokeo mazuri kwa Zanzibar na Muungano wa Comoro kwa kufikia hatua ya kusaini makubaliano ya ushirikiano kati ya nchi mbili hizo, ambayo ni matokeo ya mashauriano ya muda mrefu kati ya Zanzibar na Muungano wa Comoro.

Kwa mara ya kwanza mazungumzo yalifanyika Ikulu ya Migombani Zanzibar wakati Rais Dk. Dhonine Ikililou alipokuwa Zanzibar kushiriki Maadhimisho ya Miaka 50 ya Mapinduzi kufuatia mwaliko kutoka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mara nyingine ilikuwa katika visiwa vya Samoa wakati wa Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Nchi za Visiwa Vidogo Zinazoendelea (SIDS) ambapo viongozi hao wawili walihudhuria mkutano huo.

Mara ya tatu viongozi hao walikutana mwanzoni mwa ziara ya Rais Dk. Shein nchini humo ambapo mazungumzo yao yalizingatia namna bora zaidi ya kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya sasa na pia kuangalia maeneo mapya ya ushirikiano.

Alizungumza na Watanzania wanaoishi nchini humo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema, urafiki kati ya watu wa Zanzibar na Comoro si wa kupita bali ni udugu wa dhati na wa damu ambao umedhihirishwa na masimulizi na maandishi mbalimbali na ukaribu wao hadi hivi sasa.

"madhumuni ya ziara yangu ni kuendeleza ushirikiano wetu. Tunataka uwe (ushirikiano) na nguvu zaidi na tuuendeleze kwa kasi zaidi" alisema Dk. Shein.

Alisisitiza kuwa wakati Serikali za pande zote mbili zikianisha maeneo mapya ya ushirikiano rasmi, wananchi kwa upande wao nao hawana budi kuyaendeleza mambo ambayo walikuwa wakishirikiana kutokana na udugu na urafiki wao.

Chini ya makubaliano hayo yaliyotiwa saini mjini Moroni, Zanzibar na Muungano wa Comoro zitashirikiana katika maeneo tisa ambayo ni elimu, afya, usafiri wa baharini, habari na utamaduni, utalii, kilimo, biashara, uvuvi na masuala ya dini.

Makubaliano hayo yatazipa nchi mbili hizo fursa za kubadilishana wataalamu na uzoefu katika nyanja mbalimbali zikiwemo utafiti katika masuala ya mazingira, uvuvi, kilimo na afya. Pamoja na hayo ushirikiano katika elimu utajumuisha kupata fursa kwa vijana wa Comoro kujiunga na vyuo vya Zanzibar kujifunza fani mbalimbali katika ngazi tofauti za mafunzo.

Aidha, makubaliano hayo yanatoa fursa kwa vijana wa Zanzibar kupata nafasi za masomo hasa kujifunza lugha ya kifaransa ambayo ndio inayotumika nchini Comoro. Ni ukweli kuwa Zanzibar inahitaji wataalamu wa lugha ya kifaransa kwa ajili ya mawasiliano katika shughuli mbalimbali na hasa ikizingatia ushirikiano wake na visiwa vya bahari ya hindi ambavyo vingi vyao vinazungumza lugha ya kifaransa na katika biashara ya utalii ambayo inaendelea kuwa msingi mkuu wa uchumi Zanzibar.

Kwa upande wa Habari na utamaduni, makubaliano hayo yanawapa fursa wafanyakazi wa vituo vya Redio na Televisheni vya nchi mbili hizo kubadilishana uzoefu katika utangazaji na utayatarishaji wa vipindi pamoja na watumishi wa vituo vya redio na televisheni vya Comoro kujifunza lugha ya Kiswahili kuimarisha uwezo wao katika lugha hiyo ili kuweza kurusha matangazo na vipindi vingi kwa lugha ya kiswahili. Hatua hiyo inatarajiwa kuimarisha matumizi ya lugha Kiswahili nchini Comoro ambako wananchi wake wengi wanaifahamu lugha hiyo ingawa hawaizungumzi kwa ufasaha kama inavyozungumzwa hapa Zanzibar.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk.Ali Mohamed Shein akisalimiana na Mashekhe na Waisalmu mbali mbali alipowasili katika Msikiti Mkuu wa Mitsamihouli akiwa katika ziara ya kiserikali Comoro kwa mualiko wa Rais wa Comoro Dk Ikililou Dhoinine, tarehe 15 Septemba 2014*

Kwa upande wa utalii, Comoro inatarajiwa kunufaika na uzoefu wa Utalii wa Zanzibar ambako sekta hiyo tayari inaelekea kuwa sekta mama kutokana na kuchangia zaidi ya asilimia 27 ya pato la Zanzibar.

Kwa kuwa Zanzibar na Comoro ni washiriki katika Mpango wa Magharibi ya Bahari ya Hindi na Changamoto za Ukanda wa Pwani ambao una fursa ya kushirikiana katika sekta ya utalii, nchi hizo mbili kwa kuungana na washiriki wengine ambao ni Shelisheli, Madagascar na Reunion, zinaweza kufanya vizuri katika kuimarisha utalii katika nchi zao.

Akijibu maswali ya waandishi wa habari katika mji wa Mitsamihouli, Dk. Shein alieleza kuwa Comoro na Zanzibar zina nafasi sawa kuendeleza utalii, hivyo wao (Comoro) wanapaswa kuhimiza uwekezaji na kujitangaza kama inavyofanya Zanzibar.

Kitu kingine ambacho makubaliano hayo yatafaidika nacho katika sekta ya utalii ni ule mpango uliobuniwa hivi karibuni ujulikanao kama 'Visiwa vya Vanila' ambao umeleta dhana mpya ya kushirikiana na kuimarisha utalii katika visiwa vya ukanda huu wa bahari ya Hindi ikiwemo safari za meli za kitalii.

Ifahamike kuwa, makubaliano haya yamekuja kufuatia Comoro kurejea katika hali ya utulivu na amani baada ya sintofahamu ya muda mrefu ambapo Umoja wa Afrika ulishiriki kikamilifu katika kurejesha utulivu nchini humo na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama mwanachama wa Umoja huo ilikuwa mstari wa mbele kwenye harakati za kuleta amani nchini humo.

Lakini ni muhimu vile vile kutambua kuwa hali ya utulivu nchini humo imechangiwa na wananchi wenyewe na viongozi wao. Katika hotuba yake wakati wa dhifa ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na mwenyeji wake, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Shein alimsifu Rais wa Comoro Dk. Dhonine kwa kuiongoza nchi yake katika hali ya amani na utulivu na kuwashukuru pia wananchi wa nchi hiyo kwa kuiunga mkono Serikali yao kwa kila namna.

"Najisikia niko nyumbani kwa sababu uhusiano wetu umeimarishwa zaidi na mahusiano ya wananchi wetu kwa karne nyingi, mahusiano ambayo yamekuwa katika masuala ya kijamii, utamaduni, biashara na mambo mengine mengi" alisema Dk. Shein alipokuwa akizungumza kwenye dhifa maalum ya chakula cha jioni nchini Comoro.

Zanzibar na Comoro zina malengo yanayofanana ya kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi wao. Hiyo ni fursa adhimu kwa pande hizo mbili kushirikiana kutimiza malengo yao kwa mashirikiano ya pamoja njia ambayo ndio mwelekeo wa sasa duniani ambapo watu hujikusanya pamoja kukabiliana na changamoto zinazowakabili.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa na viongozi wengine wa kitaifa wakiwa wamesimama kwenye Swala ya Eid el Hajj iliyosaliswa na Sheikh Ali Kasiim Haji kwenye Uwanja wa Mpira Konde Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, tarehe 5 Oktoba 2014*

# Amani, utulivu ndio msingi wa maendeleo - Dk. Shein

Suala kuhusu amani, utulivu na usalama limeendelea kuwa agenda kubwa miongoni mwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla. Suala hilo limeonekana kuchukua uzito maalum katika hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein aliyoitoa kwenye Baraza la Eid el Hajj lililofanyika katika Chuo cha Kiislamu kilichoko Kiuyu, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika makala hii, Jarida la Ikulu linaelezea kwa undani zaidi suala la amani kama lilivyozungumzwa naye Mheshimiwa Rais na masuala mengine kwenye hotuba yake.

Kama ilivyokuwa kwenye sherehe nyangine rasmi za Kiserikali, sherehe za mwaka huu zilifana na zilihudhuriwa na viongozi wengi wakuu wa kitaifa wakiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Idd, Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Pandu Ameir Kificho, Kadhi Mkuu wa Zanzibar Sheikh Khamis Haji na viongozi wengine kadhaa wa dini, vyama vya siasa, Serikali pamoja na wananchi.

Ingawa hotuba ya Rais wa Zanzibar ilisheheni mambo mengi, suala la amani kwa umuhimu wake lilichukua nafasi ya pekee kutokana na ukweli kwamba bila ya amani mafanikio makubwa ambayo Serikali na jamii kwa jumla imekuwa ikijivunia, yasingeweza kupatikana.

Dk. Shein alisema kuwa Tanzania imefikia kuwa nchi ya amani kutokana na misingi ya uongozi bora iliyowekwa na viongozi wa awamu zote zilizopita na kusisitiza kuwa kila mmoja ana wajibu wa kufurahia baraka zilizopo nchini na kufanya jitihada ili kuilinda neema na kheri hiyo iliyopo.

Kwa kutambua umuhimu wa amani na utulivu katika maendeleo ya nchi hii, Alhaj Dk. Shein aliwataka wananchi kujiepusha na mifarakano na mizozo isiyokuwa na faida yoyote na alitoa wito kwa wananchi kuacha kuingiza ubinafsi wakati wanapopewa nafasi katika masuala yanayohusu jamii hasa mambo ya siasa na dini.

"Wale wote wanaofanya hivyo, watambue kuwa wanafanya makosa kwa kufikiri kwamba wana uwezo zaidi kuliko wengine wa kuondosha matatizo katika jamii kwa kutumia nguvu zao.........ni vyema tukaelimishana juu ya mema na mabaya kwa busara, badala ya kiburi na dharau", alisema Alhaj Dk. Shein.

"Tuendelee kujenga imani yetu na kumuabudu Mwenyezi Mungu hadi mwisho wa uwezo wetu, bila ya kuchoka au kutosheka; ili atukubalie sala na dua za kuitakia nchi yetu iendelee kuwa na amani, umoja, mshikamano na maendeleo"

Aidha, Dk. Shein aliwataka wananchi kutosahau kamwe, kwamba amani na umoja ni misingi ya uhai wa nchi hii na kuwataka waumini na wananchi kwa jumla kuepuka kushabikia mambo yanayokwenda kinyume na maadili mema. Alisisitiza kuwa Serikali zote mbili zitasimamia hali ya amani na utulivu kwa uwezo wake wote kwa kutambua kwamba hakuna mbadala katika suala la amani.

Maelezo na msisitizo wa Rais wa Zanzibar kwenye hotuba yake kuhusiana na suala la amani, yanatokana na ukweli kwamba Zanzibar na Tanzania kwa jumla zinahitaji sana



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitoa hotuba kwenye Baraza la Eid el Hajj lililofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Kiislamu Kiuyu Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, tarehe 5 Oktoba 2014*

kuzidi kuendelezwa kwa hali ya umoja na mshikakamano kwani ndio siri kubwa ya mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha amani, ustawi wa uchumi na kukuza maendeleo ya jamii.

Katika hotuba yake hiyo, Rais wa Zanzibar alielezea masikitiko yake makubwa kutokana na ongezeko kubwa la ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikisababisha vifo vya watu wengi wasiokuwa na hatia na kuwaacha wengine kubaki kuwa walemavu.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Jeshi la Polisi Zanzibar zinazohusiana na ajali za barabarani, kuanzia mwezi wa Januari hadi Agosti mwaka 2014 kumeripotiwa ajali za barabarani 314 zilizohusisha magari na kusabisha vifo vya watu 53 na majeruhi 377. Matukio yaliyohusisha waendesha vyombo vya moto vya maringi mawili katika kipindi hicho ni 112 na kusababisha vifo vya watu 25 na majeruhi 161.

Kufuatia hali hiyo, wananchi wengi wamekuwa wakisikitishwa na mwendo wa kasi unaofanywa na baadhi ya madereva wa magari makubwa bila ya kuzingatia waendeshao magari madogo, vyombo vingine vya moto na wanaotembea kwa miguu barabarani, mambo ambayo yanatajwa kuwa ni miongoni mwa vyanzo vya ajali hizo. Alhaj Dk. Shein aliziagiza taasisi zote zinazohusika na usalama barabarani kuyafanyia kazi manung'uniko hayo ya wananchi na kulitaka Jeshi la Polisi kuweka mikakati ya kukabiliana na matukio ya ajali kutoka kwa madereva wanaokiuka sheria na vyombo vya usafiri wa barabarani nchini ambavyo ndio vyanzo vya ajali za barabarani.

"........hatuwezi kuwaruhusu madereva wasiojali utu kuendelea kukiuka sheria na kusababisha ajali" alisisitiza Dk. Shein.





*Viongozi mbali mbali wa Kitaifa wakifuatila hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliyoitoa kwenye Baraza la Eid el Hajj lililofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Kiislamu Kiuyu Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, tarehe 5 Oktoba 2014*

# Zanzibar itakavyonufaika na mpango wa kimataifa wa kukabiliana na tabianchi

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alishiriki katika uzinduzi wa Mpango wa Magharibi ya Bahari ya Hindi wa Changamoto za Ukanda wa Pwani na Mabadiliko ya Tabianchi- WIO – CC huko Apia, mji mkuu wa visiwa vya Samoa. Makala hii inaeleza pamoja na mambo mengine, umuhimu wa mpango huo kwa mustakabala wa nchi za visiwa kama Zanzibar.

Mpango wa Magharibi ya Bahari ya Hindi wa Changamoto za Ukanda wa Pwani na Mabadiliko ya Tabianchi unashirikisha nchi za visiwa za ukanda huu ambavyo ni Seychelles, Comoro, Mauritius, Reunion na Zanzibar.

Mpango huu ni mkakati mpya wa kiutekelezaji miongoni mwa nchi za visiwa vidogo vya eneo la ukanda wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi katika kusimamia malengo ya maendeleo endelevu kwa nchi hizo.

Malengo makubwa ya Mpango huu yameelekezwa zaidi katika uhifadhi na usimamizi wa pamoja wa mazingira ya visiwa, fukwe, na bahari zake pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mpango huu unafanana kwa malengo na muundo wake na mipango mingine ya kanda nyingine za bahari duniani kwa mfano Mpango wa Changamoto za Ukanda wa Pwani wa Micronesia (Micronesia Challenge) unaojumuisha nchi za Visiwa vya Palau, Federated States of Micronesia, Marshall Islands, Guam na Northern Mariana Islands na Mapango kama huo wa Ukanda wa Caribbean (Caribbean Challenge Initiative) ambao unashirikisha Visiwa vya Bahamas, Dominican Republic, Jamaica, St. Vincent and the Grenadines, St. Lucia, Grenada, Antigua & Barbuda, St Kitts & Nevis.



*Dk. Aboud Suleiman Aboud Jumbe kutoka Idara ya Mazingira katika Ofisi ya makamo wa Kwanza wa Rais alipokuwa akitoa mada katika moja ya mikutano midogo midogo uliozungumzia Mpango wa Kimataifa wa kukabiliana na mabadilko ya tabianchi wakati Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Visiwa uliofanyika Apia Samoa, tarehe 03 Sept 2014*

Programu za Mipango hii mitatu makhsusi kwa nchi za visiwa vidogo inaungwa mkono na kufadhiliwa kwa kiwango kikubwa kupitia taasisi ya kimataifa iitwayo Global Island Partnership (GLISPA). Taasisi hii inafanya kazi chini ya mwamvuli wa Umoja wa nchi za SIDS duniani na inakwenda sambamba na utekelezaji wa Mkataba wa (Convention on Biological Diversity) unaotilia mkazo hifadhi ya mazingira na bioanuwai zikiwemo za nchi za visiwa vidogo duniani.

Kwa hivyo ni mipango inayohitaji kuungwa mkono na kila nchi na wananchi wa nchi washiriki wa mipango hii kwa kuwa kutekelezwa kwa ukamilifu kwa malengo hayo kutatoa matokeo muhimu katika kuweka mustakbala wa nchi hizo na ustawi wa wananchi wake.

Katika hotuba yake wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Magharibi ya Bahari ya Hindi wa Changamoto za Ukanda wa Pwani na Mabadiliko ya Tabianchi mbele ya viongozi wa mbalimbali wa nchi za visiwa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alielezea umuhimu wa mpango huo na kusisitiza msimamo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuunga mkono mpango huo.

Katika hotuba yake hiyo, Dr. Shein alieleza kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaamini kuwa Mpango huo ni chombo muafaka/maridhawa katika kuleta maendeleo endelevu katika nchi hizo.

"Mpango huu unatoa fursa kwa washiriki walio katika mazingira yanayofanana kufanyakazi kwa pamoja katika kubuni na kutekeleza mikakati ya pamoja kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi" alisema Rais wa Zanzibar.

Aliongeza kuwa kufanyika kwa uzinduzi wa Mpango wa WIO-CC sambamba na Mkutano wa Nchi za Visiwa Zinazoendelea (SIDS) wenye kuhimiza maendeleo endelevu ni fursa nyingine kwa nchi wanachama wa Mpango huo kufanya masuala yao kueleweka miongoni mwa Jumuiya ya Kimataifa.

Aliwaeleza wageni waliohudhuria uzinduzi huo wakiwemo viongozi mbalimbali kutoka taasisi za kikanda za nchi za visiwa kuwa ni bahati iliyoje kwa uzinduzi huo kuhudhuriwa na



*Dk. Aboud Suleiman Aboud Jumbe kutoka Idara ya Mazingira katika Ofisi ya makamo wa Kwanza wa Rais alipokuwa akitoa mada katika moja ya mikutano midogo midogo uliozungumzia Mpango wa Kimataifa wa kukabiliana na mabadilko ya tabianchi wakati Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Visiwa uliofanyika Apia Samoa, tarehe 03 Sept 2014*

wageni wengi na taasisi mashuhuri zinazoshughulikia maendeleo duniani. Ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mpango huo kunaiwezesha Zanzibar kupata fursa ya kutumia mifuko mbali mbali ya kimataifa inayohusiana na Bioanuwai, Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Mipango ya Maendeleo Endelevu.

Aidha, ushiriki huo unaiwezesha pia Zanzibar kupata misaada mbali mbali ya kifedha, kitaaluma, kiufundi, na teknolojia, kupitia moja kwa moja katika mukhtadha wa maendeleo endelevu ya nchi za visiwa vidogo.

Wakati tukizungumzia uzinduzi wa Mpango huo hatuna budi pia kutoa maelezo machache kuhusu ushiriki wa Zanzibar katika mradi mwingine ulio na mafungamano na ushirikiano wa ukanda huu ambao unajulikana kama mradi wa visiwa (ISLANDS Project).


Mradi huu ambao awali haukuishirikisha Zanzibar, ulianzishwa kwa lengo la kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mkakati wa Mauritius ambao ulianzishwa kwa ajili ya nchi wanachama wa Kamisheni ya Bahari ya Hindi ambao ni Comoro, Madagascar, MauritIus na Re Union. Hata hivyo, Zanzibar ilipata bahati ya kuingizwa katika mradi huo kutokana na mapendekeo ya Kamisheni ya Bahari ya Hindi ambayo kama ilivyoelezwa awali ndio inayofadhili miradi katika ukanda huu.

Maamuzi ya Kamisheni hiyo yalizingatia malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu nchi za SIDS pamoja na mazingira halisi ya Zanzibar kama vile changamoto za kimazingira, jiografia na hali ya uchumi na kijamii pamoja na historia inayofanana na ya nchi za visiwa mwanachama mradi huo.

Lakini jambo la kujivunia ambalo lilichangia Kamisheni kuikaribisha Zanzibar katika mradi huo ni mafanikio makubwa iliyopata Zanzibar katika kutekeleza mradi wa Kikanda wa Usimamizi wa Maliasili za Ukanda wa Pwani (ReCoMaP).

Ushiriki wa Zanzibar katika Mpango wa Magharibi ya Bahari ya Hindi wa Changamoto za Ukanda wa Pwani na Mabadiliko ya Tabianchi na Mradi wa ISLANDS unatokana na ukweli kuwa utekelezaji wake unachangia katika kufanikisha baadhi ya malengo ya mipango yetu ya maendeleo ikiwemo Dira ya Zanzibar 2020 na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini Awamu ya Pili -MKUZA II.

Miongoni mwa viongozi hao ni pamoja na Rais wa Visiwa vya Palau Tommy E. Remengesau Jr., Rais wa Serikali ya Shirikisho la Visiwa vya Micronesia Emanuel Mori na Rais wa visiwa vya Marshalls Christopher Loeak. Wengine ni Waziri Mkuu wa Samoa Tuilaepa Lupesoliai Sailele Malielegaoi, Waziri Mkuu wa Grenada Dr. Keith Mitchell na Waziri wa Mambo ya Nje wa Seychelles Jean-Paul Adam.



*Baadhi ya wajumbe wa moja ya mikutano midogo midogo iliozungumzia Mpango wa Kimataifa wa kukabiliana na mabadilko ya tabianchi wakati Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Visiwa uliofanyika Apia Samoa, akiwepo Mkurugenzi Idara ya Mazingira Sheha Mjaja Juma, tarehe 03 Sept 2014*

# Matukio katika Picha



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Rais wa Comoro Dk. Ikililou Dhoinine tarehe 02 Septemba 2014 wakati waliposhiriki katika Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Nchi za Visiwa uliofanyika Apia Samoa hivi karibuni*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na Mkewe Mama Mwanamwema Shein walipokuwa wakipata maelezo kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Muungano wa Visiwa vya Comoro El-Anrif Said Hassane wakati walipotembela Ufukwe wa Mji wa Mitsamihouli walipokuwa katika ziara ya Kiserikali Comoro, tarehe 15 Septemba 2014*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein (katikati) akiwa na Makamu wake wawili Maalim Seif Sharif Hamad na Balozi Seif Ali Iddi wakiwa katika ukumbi wa Skuli ya Chwaka Jimbo la Tumbe Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba alipofika kuwasalimia Mashekhe na Wazee wa Wilaya hiyo mara baada ya Swala ya Eid el Hajj, tarehe 5 Oktoba 2014*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na waandaaji maonesho ya kilele cha maadhimisho ya siku ya usafiri wa Majini katika viwanja vya Ukumbi wa Salama Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja, tarehe 25 Septemba 2014*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na mkewe Mama Mwanamwema Shein mara baada ya kutoa hotuba katika sherehe za Baraza la Eid el Hajj lililofanyika katika ukumbi wa Skuli ya Kiuyu Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba akiwa ambapo mgeni rasmi alikuwa ni, tarehe 05 Oktoba 2014*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa katika picha ya pamoja na ujumbe wa Benki ya Biashara NBC ulioongozwa na Ms Mzimga Melu (kushoto waliokaa) tarehe 22 Septemba 2014*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitoa hotuba kwenye kilele cha miaka 50 ya Elimu bila Malipo katika Kiwanja cha Amani Zanzibar, tarehe 23 Septemba 2014*

# Miaka 50 ya elimu bila ya malipo

## ▪ Huduma za elimu zimekua sambamba na ongezeko la idadi ya watu

Wakati wananchi wa Zanzibar wakiadhimisha miaka 50 tokea kutangazwa elimu bila ya malipo nchini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa fahari kubwa inatangaza mafanikio yaliyopatikana kwenye sekta hiyo na kuhakikisha kuwa mahitaji ya elimu kwa kiasi kikubwa yanakwenda sambamba na ongezeko la idadi ya watu.

Tarehe 23, Septemba 2014, ni miaka 50 tokea Rais wa kwanza wa Zanzibar na Jemadari wa Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964 Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, alipotoa tamko la kutekeleza ahadi ya Afro Shirazi Party (ASP) la kutoa elimu bila ya malipo kwa wananchi wote wa Zanzibar bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Tamko hilo ndilo lililokuwa mkombozi mkubwa wa watoto wa wanyonge kupata nafasi ya elimu na kuweza kuendesha nchi yao bila ya ubaguzi.

Kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964, elimu Zanzibar ilitolewa kwa misingi ya ubaguzi kwa dhamira ya kupata makarani wachache wa kuutumikia utawala uliokuwepo. Skuli zilizokuwepo kwa wakati huo zilikuwa ni chache na kamwe hazikuweza kutosheleza mahitaji ya watoto waliokuwepo.

Takwimu zinaonesha kuwa kulikuwa na jumla ya skuli mbili tu za maandalizi, 62 za Msingi zilizokuwa na wanafunzi 19,106 na skuli nne tu za Sekondari za Serikali zilizokuwa na wanafunzi 734. Watu maalum kutoka kwenye familia za watawala ndio waliokuwa wakifaidika zaidi na huduma hiyo huku wanyonge watoto wa wakwezi na wakulima wakibaki bila ya kusoma. Hali hiyo ni tofauti na leo ambapo kuna jumla ya skuli za maandalizi 279 zenye wanafunzi 46,880, skuli za msingi 359 zenye jumla ya wanafunzi 252,938 na skuli za sekondari 256 zenye jumla ya wanafunzi 81,757.

Vile vile, asilimia ya uandikishaji katika ngazi ya elimu ya maandalizi imefikia asilimia 30.9, msingi asilimia 100 na asilimia 59.90 katika ngazi ya sekondari; kidato cha Kwanza hadi kidato cha Nne.

Ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na upatikanaji wa walimu wa kutosha na wenye uwezo unaohitajika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza idadi ya vyuo vya kutoa mafunzo ya ualimu Unguja na Pemba. Aidha, Serikali imeanzisha vyuo vikuu vyake vitatu ambavyo vinatoa mafunzo katika fani mbali mbali katika ngazi ya Kimataifa. Jitihada mbali mbali zinaendelezwa za kuviimarihsa vyuo vikuu hivyo pamoja na kutanua wigo wa mafunzo yanayotolewa.

Moja miongoni mwa hatua za kujivunia katika vyuo hivyo ni pamoja na kufikia hatua ya kuanza kutoa Shahada ya Uzamifu (PhD) ya Kiswahili hapa Zanzibar katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) jambo ambalo limeipa heshima kubwa Zanzibar katika maendeleo ya elimu ya juu. Vile vile,



*Wanafunzi kutoka skuli mbali mbali za Zanzibar wakiimba wimbo maalum wa sherehe za Elimu bila Malipo kutimia miaka 50 katika Kiwanja cha Amani Zanzibar, tarehe 23 Septemba 2014*



*Wanafunzi wa Chuo cha Kiislamu wakipita mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein wakiwa kwenye maandamano ya sherehe za Elimu bila Malipo kutimia miaka 50 katika Kiwanja cha Amani Zanzibar, tarehe 23 Septemba 2014*

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimeanza kutoa mafunzo ya udaktari kuanzia mwaka jana ambapo jumla ya wanafunzi 33 wamejiunga na masomo hayo. Matarajio ya Serikali ni kwamba Zanzibar itakuwa na madaktari wa kutosha katika miaka michache ijayo.

Ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na teknolojia, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kutoa mafunzo mbali mbali ya kiufundi kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia pamoja na vituo vitatu vya Mafunzo ya Amali vilivyopo nchini. Jitihada za Serikali za kushajihisha wawekezaji katika sekta ya elimu zimekuwa zikizaa matunda mazuri ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa taasisi nyingi za elimu zinazomilikiwa na watu binafsi kuanzia ngazi ya maandalizi hadi elimu ya juu. Hayo ni mafanikio ya kupigiwa mfano yaliyopatikana katika miaka hii 50 ambayo yametokana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuinua elimu nchini na kuendeleza azma ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ya kuwapatia fursa mbali mbali za elimu watoto wa Zanzibar.

Kutokana na kutambua umuhimu wa elimu kwa maendeleo, suala la uimarishaji wa elimu limepewa kipaumbele katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II), Mpango wa Maendeleo ya Elimu pamoja na Malengo ya Milenia ya Elimu.

Miongoni mwa mambo yaliyodhamiriwa katika utekelezaji wa mipango hii ya maendeleo ni pamoja na kuhakikisha kuwa mpango wa upatikanaji wa elimu ya lazima ya miaka 12 kwa watoto wote unatekelezwa, kunakuwa na usawa na haki katika utoaji wa elimu na ubora wa elimu inayotolewa unaongezeka na kuimarishwa.

Mambo mengine yaliyopewa kipaumbele kushughulikiwa ni kuhakikisha kuwa raslimali zinazotengwa kwa ajili ya utoaji wa elimu zinatumika kwa ufanisi na kwa kuyatimiza malengo yanayokusudiwa, asasi za uongozi na uendeshaji wa sekta ya elimu zinaimarishwa na wahusika mbali mbali wa elimu ikiwemo sekta binafsi katika upangaji na utekelezaji wa sera ya elimu wanashirikishwa.

Ni dhahiri kwamba wananchi wa Zanzibar wanayo kila sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopatikana katika kuendeleza elimu nchini. Ni jukumu la kila mtu kuyaenzi, kuyadumisha na kuyaendeleza mafanikio hayo.



*Wanafunzi wa Skuli mbali mbali wakinyanyua picha za Mawaziri walioiongoza Wizara ya Elimu kwa vipindi tofauti mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwenye kilele cha sherehe za Elimu bila Malipo kutimia miaka 50 katika Kiwanja cha Amani Zanzibar, tarehe 23 Septemba 2014*

Ili kuhakikisha kuwa mafanikio hayo yanakuwa endelevu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya kila juhudi kuona kuwa skuli zaidi za msingi zinajengwa kwa kushirikiana na wananchi na kuendelea kukamilisha ujenzi wa madarasa yanayoanzishwa na wananchi kwa kutambua kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kukabiliana na changamoto ya uchache wa madarasa katika baadhi ya skuli au umbali wa skuli katika baadhi ya maeneo.

Ujenzi wa Skuli mpya 21 za sekondari katika kila Wilaya ambapo hivi sasa skuli 19 tayari zimeshakamilika umetanua fursa za kujiunga na elimu ya sekondari kwa wanafunzi wa Zanzibar.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya elimu bila ya malipo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, amewahakikishia Wananchi wa Zanzibar kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza dhamira yake ya kuifanya elimu ya sekondari hadi kidato cha Nne kuwa ni ya lazima ifikapo mwaka 2020 na kuongeza kuwa lengo ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaweza kupata elimu ya lazima ya miaka 12 hadi Kidato cha Nne.

Sambamba na kuongeza upatikanaji wa nafasi za kusomea, Serikali inafanya juhudi kubwa katika kuhakikisha kuwa ubora wa elimu nchini unazidi kuongezeka. Juhudi zaidi zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuzipatia skuli vifaa na nyenzo za kisasa za kufundishia ikiwemo vitabu, vifaa vya maabara, kompyuta na walimu waliobobea ili wanafunzi waweze kufanya vizuri zaidi.

Amesisitiza umuhimu wa wanafunzi kuongeza bidii katika kujifunza masomo yote na kuendelea kutilia mkazo katika masomo ya Sayansi na Teknolojia, kwani masomo hayo ndio yenye nafasi kubwa katika shughuli za kila siku katika karne hii ya 21 ambayo inaitwa karne ya Sayansi na Teknolojia.



# Kuwaenzi, kuwaheshimu wazee uwe utamaduni endelevu Zanzibar

Zanzibar kama yalivyo mataifa mengine duniani, imetenga maeneo maalum ya kuwahifadhi wazee wasiojiweza na watu wanaoishi katika mazingira magumu kwa lengo la kuwaenzi na kuwatunza watu hao na hivyo kurahisisha njia za kuwapatia huduma muhimu za kijamii wakiwa kwenye makazi yao.

Mchango wa wazee kwa njia moja au nyengine umesaidia kuleta maendeleo ya nchi na ndio chimbuko la vijana wa leo. Watu wenye kuishi katika mazingira magumu nao wanayo kila sababu ya kutambuliwa rasmi ili iwe rahisi kwao kufikiwa kila haja ya kufanya hivyo inapotokea.

Utamaduni wa kuwaenzi wazee na watoto yatima ni miongoni mwa mambo muhimu yanayomjengea heshima mwanadamu duniani na hasa katika bara la Afrika.

Ingawa utamaduni wa kuwahamisha wazee kuwapeleka kwenye nyumba zao maalum umezoeleka katika mataifa yaliyoendelea kiasi ambacho wazee na watoto wao wameshajengeka kisaikolojia kwamba unapofikia umri wa kuhamia kwenye nyumba zao hizo haiwapi usumbufu kufanya maamuzi, baadhi ya mataifa ya Bara la Afrika ikiwemo Zanzibar, suala hilo bado linaonekana halijazoeleka sana miongoni mwa jamii. Bado waliowengi wanaamini kwamba mzee mwenye watoto wake hawezi kupelekwa kwenye makaazi hayo wakiamini kwamba kufanya hivyo ni kumtelekeza mzee.

Uamuzi wa kuwatengea makaazi wazee ni heshima kubwa kwao na hiyo ni moja miongoni mwa sababu zilizoifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchukua uamuzi wa kujenga nyumba za wazee katika maeneo ya Sebleni Unguja na Limbani kule Pemba mara tu baada ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964. Hatua ya Serikali ya kujenga nyumba hizo ilichukuliwa kutokana na kutambua kuwa wazee ni chemchem ya busara katika jamii na ndio chimbuko la familia.

Kwa kutambua heshima ya wazee, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar



*Mama Mwanamwema Shein*
*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi*




*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein akikabidhi misaada mbali mbali kwa wazee wa kijiji cha Matemwe, tarehe 7 Julai 2014*

katika kipindi cha miaka minne iliyopita imechukua juhudi maalum za kuwasaidia wazee wa Sebleni kwa Unguja na Limbani Pemba, ikiwa ni miongoni mwa jitihada zake (serikali) za kuwapatia hifadhi ya makaazi, huduma bora za afya na misaada mingine ya kijamii.

Matukio mbali mbali ya kuwasaidia wazee kwenye nyumba hizo yanayofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mkewe Mama Mwanamwema Shein siyo tu wanayafanya kwa sababu ya kutekeleza malengo ya Serikali pekee, lakini vile vile ni utamaduni wa Wazanzibari wa kuwaenzi na kuwaheshimu wazee.

Katika hali isiyo ya kawaida yapo baadhi ya maeneo nchini Tanzania ambako kumeibuka itikadi potofu za kuwadhalilisha wazee kutokana na maumbile yao hali ambayo imekuwa ikihatarisha pia maisha yao.

Kumekuwa na imani kwenye maeneo hayo za kuwahusisha wazee wenye macho mekundu na imani za kishirikina. Inaaminika kwamba watu waliobahatika na maumbile hayo wanahusishwa na mambo ya uchawi na hivyo kuuawa kikatili. Zipo kesi chache zinazohusishwa pia na mambo hayo hapa Zanzibar. Aidha, wapo baadhi ya watu wenye kuwakimbia wazazi wao kutokana na imani hizo. Hizi ni itikadi potofu ambazo hazinabudi kulaaniwa kwa nguvu zote.

Wenye kufanya vitendo hivyo vya kikatili dhidi ya wazee, wanapaswa kufahamu kwamba wanafanya vitendo vibaya ambavyo siyo tu ni kinyume na sheria za nchi, lakini vile vile ni vitendo vinavyokwenda kinyume na haki za kibinadamu na pia vinamchukiza Mwenyezi Mungu.

Wanapaswa kufahamu kwamba kila mtu anayo haki ya kuheshimiwa, kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake. Aidha, imeelezwa kwenye sheria za nchi hii kwamba kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka katika Serikali na jamii kwa mujibu wa sheria za nchi.

Vyombo vya sheria havina budi kusimamia ipasavyo sheria za nchi kuzuia mauaji ya kikatili dhidi ya wazee vikijua kuwa vina wajibu wa kuzingatia na kuhifadhi haki za binadamu ikiwa ni msingi wa uhuru kama ilivyoainishwa katika sheria za nchi, na kwamba kila mtu anayo haki ya uhuru wake kuthaminiwa, kuheshimiwa, kuhifadhiwa na kudumishwa na mamlaka ya nchi, taasisi binafsi na kila mwananchi.

Ingelikuwa na tija sana iwapo jamii ingeliweza kuchukua hatua za kuwaenzi wazee kwa kuwapatia misaada mbali mbali ya kibinadamu ambayo itawaletea faraja katika kipindi chao cha maisha ya uzeeni kama inavyofanywa na baadhi ya viongozi serikalini na vile vile baadhi ya jumuiya za kiraia.

Juhudi anazozichukua Mama Mwanamwema Shein za kuwapatia misaada mara kwa mara wazee na watoto yatima katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba, hazina budi kuchukuliwa kuwa mfano mzuri wa kuigwa na kila mwanadamu mwenye kujali utu, imani, heshima na upendo kwa binadamu wenzake.

Mama Mwanamwema ambaye ni Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amejijengea utamaduni wa kuwafariji wazee na watu wengine wenye kuishi katika mazingira magumu akijua kuwa kwa kufanya hivyo siyo tu kunamjengea hatma njema ya maisha yake ya baadae, bali ni jukumu lake kama binadamu kuwatizama wale ambao kwa njia moja au nyengine wanahitaji msaada kutoka kwa wengine.

Hatua hii imeweza kumjengea heshima kubwa mbele ya jamii, na ni Mwenyezi Mungu pekee ndiye ajuaye cha kumlipa mja wake huyu kutokana na amali yake hiyo njema anayoifanya kwa binadamu wenzake.



*Wahitimu wa mafunzo ya Udaktari wa Binadanu wakiwa katika Mahfali ya Kwanza ya Chuo cha Madaktari Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Mbweni nje ya Mji wa Unguja, tarehe 28 sept 2014*

# Huduma za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar zinavyozidi kuimarika

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu inaendelea na mpango wake wa kuhakikisha kuwa kila Mzanzibari mwenye sifa na fursa ya kusoma Elimu ya juu anaitumia fursa hiyo kwa kuwapatia Wazanzibari fedha za gharama za masomo kwa njia ya mkopo ambao urejeshwaji wake hauna riba.

Kama ilivyoainishwa katika ibara 84(e) ya Ilani ya uchaguzi ya CCM 2010/2015, Serikali imeitaka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuboresha utaratibu wa utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ili kukidhi mahitaji ya wataalam wanaohitajika katika sekta rasmi na sekta binafsi.

Mwenendo wa utoaji mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kuanzia mwaka 1964 hadi tarehe 30 June 2014 unaonesha kuwa umepita katika nyanja tafauti kwa vipindi tafauti. Kuanzia mara baada ya Mapinduzi 1964 hadi kufikia mwaka 2001, ufadhili huo wa masomo ulikuwa ukitolewa kwa njia ya ruzuku na si kwa njia ya mkopo kama ilivyo sasa. Vijana walikuwa wakisomeshwa na Serikali bila ya kurejesha fedha hizo.

Kufuatia mwamko mkubwa wa kielimu mwanzoni mwa miaka ya 2000, idadi ya wahitaji ilikuwa ikiongezeka kwa kasi, hali ambayo ilipelekea Serikali kupitisha sheria Nam. 6 ya mwaka 2001, ambayo imeidhinisha kuanzishwa kwa chombo rasmi kitakachotambulika kisheria kuwafadhili vijana wanaohitaji kusomeshwa Elimu ya Juu kijulikanacho Mfuko wa Elimu ya Juu.

Katika kipindi chote cha uwepo wa Mfuko wa Elimu ya Juu, kumekuweko na wimbi kubwa la ongezeko la waombaji wa ufadhili wa masomo na hivyo kuipa Serikali changamoto kubwa ya kuendelea kuwadhamini vijana wote wanaohitaji ufadhili huo kwa njia ya ruzuku.

Sera ya Elimu ya mwaka 2006 ambayo inatilia mkazo kuanzishwa kwa chombo endelevu chenye ufanisi kiutendaji kitakachosimamia Elimu ya Juu, kimekuwa ndio suluhisho la kudumu la kukabiliana na changamoto za Mfuko wa Elimu. Kutokana na sera hiyo, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lilipitisha sheria No 3 ya mwaka 2011 ya kuanzishwa kwa Bodi ya Mkopo wa Elimu ya Juu Zanzibar, hatua ambayo imewawezesha vijana wa Zanzibar kupatiwa ufadhili kwa njia ya mkopo. Chini ya utaratibu huo, mara tu baada ya mkopaji kuhitimu masomo yake na kuanza kazi, atalazimika kurejesha fedha hizo ili ziweze kutumika kuwasomesha vijana wengine.

Mfumo thabiti wa urejeshaji mkopo ulianzishwa na vijana wote waliokopeshwa kuanzia mwaka 2006 hadi kurithiwa kwa mfuko na Bodi ya mikopo walilazimika kurejesha fedha hizo.

Pamoja na kufanikiwa kwa kuanzishwa kwa mfumo wa urejeshwaji mkopo, Bodi pia imeweza kuweka Mtandao wa taarifa za wakopaji waliopata ufadhili kuanzia mwaka 2006 hadi sasa. Taarifa hizi zinatumika kuwatafuta wadaiwa ili kuanza mikato yao na kuiwezesha bodi kuongeza mfuko.

Ili kuboresha mahusiano na kuifanya Bodi itambuliwe rasmi na Taasisi za Elimu ya Juu, Bodi imeshafunga mkataba wa maelewano (MOU) na kufanya mazungumzo na vyuo mbali mbali Zanzibar, Tanzania Bara na vyuo vyengine vya nje ya nchi, hatua ambayo inawawezesha wanafunzi wanaosomeshwa kwenye vyuo hivyo kutambuliwa rasmi na kusoma bila ya usumbufu.

Katika kuitambulisha Bodi kimataifa, mchakato wa kujiunga na Jumuiya ya Bodi za vyuo vikuu vya Afrika, "The Association of African Higher Education Financing Agencies" (AAHEFA) umeshafikia hatua nzuri. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inatarajia kujifunza mambo mengi kutokana na jumuiya hiyo na hivyo kuongeza ufanisi zaidi.

Aidha, Bodi imefanikiwa kuwapatia posho la kujikimu na nauli vijana wote wanaosoma vyuo vya Zanzibar kupitia Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ), jambo ambalo limepunguza msongamano na foleni katika ofisi za Bodi na kuwapunguzia kazi watendaji wa Bodi.


Bodi ya Mikopo inaendelea na kampeni ya urejeshaji mikopo kwa wahitimu ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali linalowataka wahitimu walioajiriwa kurejesha mikopo yao ili kuipa uwezo Serikali kusomesha vijana wengine wanaohitaji mkopo huo. Tokea kampeni za urejeshaji mikopo zilipoanza na kuwatafuta vijana waliosomeshwa na Mfuko wa Elimu ya Juu kuanzia 2006 hadi 2011, kumekuwa na mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

Utaratibu wa urejeshaji wa mikopo kwa wahitimu unaanza mara tu baada ya mwanafunzi kuhitimu masomo yake na kuajiriwa. Wasioajiriwa hupewa muda hadi wanapopata ajira na kwa wale wanaojiajiri wenyewe wanatakiwa wawasilishe mikato yao katika ofisi za Bodi za Unguja na Pemba.

Hadi kufikia June 2014 zaidi ya wanafunzi 4000 wameshasomeshwa na Bodi ya Mikopo kwa kiwango cha Stashahada ya juu, Shahada ya kwanza, Shahada ya uzamili na uzamivu. Hii inaifanya Serikali kutimiza kiasi cha Shilingi bilioni 25 tangu kuanzishwa kwa mfumo wa mikopo na Mfuko wa Elimu ya Juu mwaka 2006 hadi Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Kasi ya urejeshaji wa mikopo inakua mwaka hadi mwaka kufuatia utekelezaji wa mikakati ya ukusanyaji wa fedha hizi, udhibiti na ufatiliaji wa taarifa za wakopaji. katika mwaka 2013/2014 Bodi imefanikiwa kukusanya jumla ya Tshs. 248,808,482.33/= ambayo ni ongezeko la Tshs.153,325,866.33/= kutoka kwa makusanyo ya mwaka wa fedha 2012/2013 Tshs. 95,482,616/=
Pia kwa mwaka wa fedha 2013/14 idadi ya wahitimu walioanza kurejesha mikopo yao ya masomo imeongezeka hadi kufikia wafanyakazi 453 kutoka wafanyakazi 221 kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

| **MAREJESHO 2013/2014** | | | |
|---|---|---|---|
| **SN** | **MWEZI** | **JUMLA YA WALIPAJI** | **JUMLA YA MAKUSANYO (TZS)** |
| 1 | JULAI 2013 | 257 | 15,334,254.00 |
| 2 | AGOSTI 2013 | 264 | 15,297,180.00 |
| 3 | SEPTEMBA 2013 | 296 | 21,191,235.00 |
| 4 | OKTOBA 2013 | 298 | 20,073,350.00 |
| 5 | NOVEMBA 2013 | 308 | 19,884,100.00 |
| 6 | DISEMBA 2013 | 327 | 20,863,667.00 |
| 7 | JANUARI 2014 | 334 | 21,652,221.00 |
| 8 | FEBRUARI 2014 | 355 | 18,204,895.33 |
| 9 | MACHI 2014 | 384 | 21,124,278.00 |
| 10 | APRILI 2014 | 397 | 23,245,625.00 |
| 11 | MEI 2014 | 430 | 25,885,647.00 |
| 12 | JUNI 2014 | 453 | 26,052,030.00 |
| | **JUMLA KUU** | | **248,808,482.33** |





Kufuatia kununuliwa kwa vifaa mbali mbali vya kisayansi na teknolojia, Bodi imeazimia kuanzisha mfumo wa utoaji na ujazwaji fomu za mikopo kwa njia ya mtandao kupitia kwenye tovuti yake ifikapo mwaka wa fedha 2015/2016.

Kama ilivyoagizwa, Bodi imeazimia kutafuta fursa mbali mbali na vyanzo vingine vya fedha zitakazotumika kuwafadhili wanafunzi wanaohitaji kusoma nje na ndani ya nchi kwa miaka ijayo

Bodi pia imeazimia kuboresha mfumo wa urejeshaji mikopo ili kuongeza kasi zaidi ya urejeshwaji fedha ambazo zinahitajika kwa kuwakopesha wanafunzi wengine wanaohitaji mkopo huo.

| **MAKADIRIO 2014/2015** | |
|---|---|
| **MWEZI** | **JUMLA (TZS)** |
| JULAI 2014 | 28,000,000.00 |
| AGOSTI 2014 | 29,000,000.00 |
| SEPTEMBA 2014 | 30,000,000.00 |
| OKTOBA 2014 | 34,000,000.00 |
| NOVEMBA 2014 | 34,500,000.00 |
| DISEMBA 2014 | 35,000,000.00 |
| JANUARI 2015 | 37,000,000.00 |
| FEBRUARI 2015 | 38,000,000.00 |
| MACHI 2015 | 39,000,000.00 |
| APRILI 2015 | 40,000,000.00 |
| MEI 2015 | 41,000,000.00 |
| JUNI 2015 | 45,000,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **430,500,000.00** |



# Sera ya polisi jamii imeimarisha usalama wa raia na mali zao



*Kamishna wa Polisi Zanzibar CP Hamdan Omar Makame akimkabidhi vifaa vya ulinzi mmoja kati ya wananchi wa Mwanyanya ikiwa ni hatua ya kutekeleza sera ya ulinzi shirikishi inayotiliwa nguvu na jeshi la Polisi la Tanzania, makabidhiano hayo yalifanyika tarehe 11 Februari, 2014 Mwanyanya Zanzibar*

Falsafa ya polisi jamii ambayo iliasisiwa kwa mara ya kwanza nchini Uingereza na Bwana Robert Peel kwenye miaka ya 1829, imeanza kufurahiwa hapa Zanzibar miaka michache tu baada ya kuanzishwa na kueleweka miongoni mwa wananchi.

Bwana Robert Peel ambaye alizaliwa mwaka 1750 na kufariki mwaka 1830, alikuwa Veterani wa Jeshi la Polisi la Uingereza, na anaendelea kukumbukwa nchini humo kwa kuanzisha "Metropolitan police" na kitabu chake alichokiandika kuwa "police is a people", kutokana na namna jamii inavyopaswa kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi.

Falsafa ya Afisa huyo wa jeshi la polisi ambaye alishika nyadhifa kubwa katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi hiyo, ilimaanisha kuwa jeshi la polisi ni la watu na watu ni jeshi la polisi. Falsafa hii inabainisha kuwa Jeshi la Polisi haliwezi kutekeleza majukumu yake ya kusimamia usalama wa raia na mali zao bila ya kuwashirikisha kikamilifu raia wenyewe.

Kwa karibu miaka minane sasa tokea Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipoanza kutekeleza falsafa ya polisi jamii nchini. Falsafa hiyo imeanza kueleweka miongoni mwa jamii baada ya juhudi maalum zilizochukuliwa za kuelimisha juu ya namna ya kufanyakazi kwa pamoja na jeshi hilo, na kuondokana na dhana iliyokuwa imejengeka miongoni mwa jamii, kwamba askari polisi ni mtu adui na kwamba wakati wote wananchi wa kawaida wanatakiwa kuwa na tahadhari nao na ikibidi kuwa mbali nao.

Historia inatufundisha kuwa miaka michache baada ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964, watoto watukutu katika familia nyingi walikuwa wakirekebishwa tabia zao siyo tu kwa bakora pekee, lakini vile vile kitisho cha kuitiwa askari polisi kilikuwa kikitumika mara kadhaa kwa watoto wa aina hiyo, na kimsingi ilikuwa dawa muafaka kwa watoto hao.

Ni vyema ikaeleweka kuwa maana halisi ya polisi jamii ni ushirikiano wa kila mwananchi aliyekuwemo ndani ya jamii kutengemea na nafasi aliyokuwa nayo katika suala zima la kusimamia amani na usalama. Kupitia utaratibu huu Jeshi la Polisi huingia ubia na wananchi kwa lengo la kutafuta namna bora zaidi na endelevu ya kupambana na uhalifu, kusimamia hali ya amani, utulivu na usalama wa wananchi na mali zao.

Kwa lengo la kuhakikisha azma ya kuwepo kwa utekelezaji mzuri wa sera ya Polisi Jamii, miradi mbali mbali imebuniwa ili kuona kuwa suala hili linafanikiwa kwa kuzingatia mazingira yaliyopo. Miradi hiyo ni pamoja na ulinzi Shirikishi ambao huruhusu uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi vya wananchi wenyewe katika mitaa na maeneo yao. Vikundi hivi hushirikiana na Jeshi la Polisi kuendesha doria hasa wakati wa usiku. Katika mitaa na shehia ambazo tayari wameanzisha vikundi vya aina hii wameelezea kuridhika kwao na maamuzi ya kuwepo kwake.

Bwana Juma Mahmoud wa Kwahani ameliambia Jarida la Ikulu kwamba hivi sasa wanaridhishwa na hali inayoendelea




*Wananchi mbali mbali wa Mwanyanya wakimemo na watoto wakifuatilia makabidhiano ya vifaa vya ulinzi yaliyofanywa na PC Hamdan Omar Makame kwa wananchi wa Mwanyanya tarehe 11 Februari 2014, Mwanyanya Zanzibar*

kwenye shehia yao ambapo amesema matukio ya uhalifu hasa ya wizi wa majumbani, ubakaji na udhalilishaji na mengine dhidi ya kinamama na watoto wa kike yamepungua kwa kiasi kikubwa hivi sasa ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Kauli kama hiyo imetolewa pia na Bibi Amina Suwed wa Chukwani ambaye amekaririwa akisema kuwa "kabla ya kuwepo polisi jamii tulikuwa tunaogopa kufika maeneo tunayoishi hasa inapofika wakati wa usiku, kinachotufariji sasa ni kwamba hata ukichelewa kwenye shughuli zako utakutana na polisi jamii ukijieleza vizuri wanakuelewa na tena wanakusindikiza hadi nyumbani", alisema Bibi Amina.

Katika baadhi ya maeneo vikundi hivi husaidiana na Jeshi la Polisi kusimamia usalama barabarani hasa wakati wa sikukuu. Hali hiyo inaonekana katika maeneo ya Mtoni, Meli nne – Kitosani, Daraja Bovu na maeneo mengine. Aidha, vikundi hivi husaidia katika kuimarisha ulinzi wa wageni na watalii hasa katika maeneo ya Mji Mkongwe na sehemu mbali mbali za mashamba kwenye ukanda wa bahari.

Mji mkongwe hasa katika maeneo ya Malindi, polisi jamii wanatumiwa kusaidia katika kazi za kuimarisha ulinzi wa vyombo vya moto na hata baskeli kwa wananchi wanaokwenda kununua samaki shughuli ambayo pia inaingiza mapato ndani ya shehia hiyo.

Watumiaji wa madawa ya kulevya ambao walikuwa wamesambaa kwenye maeneo ya Mikunguni Kinuni na maeneo mengine mengi yenye mfumo mzuri wa polisi jamii yameonekana kupungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kazi nzuri inayofanywa na polisi jamii.

Mradi mwengine muhimu kulingana na mazingira ya Zanzibar ni mradi wa ulinzi jirani. Kupitia mradi huu watu wanaoishi karibu au wanaofanya shuhguli zao pamoja kama wafanyabiashara huwa na jukumu ya kusimamia ulinzi na usalama wa jirani yako hasa katika wakati asiokuwepo. Mradi huu unatilia mkazo utamaduni wa watu wa Zanzibar wa hushirikiana katika masuala mbali mbali yakiwemo ya kiusalama na hata malezi ya watoto katika mitaa.

Katika wakati huu ambapo jamii inakabiliwa na tatizo ya wizi wa mazao na mifugo hasa ng'ombe katika baadhi ya vijiji, kuna haja ya kushirikiana katika kulinda mali. Watu hawanabudi kushirikiana kwa kujua kuwa limfikalo mmoja leo, kesho ni zamu ya mwengine. Hivyo, inampasa kila mmoja na hasa kila mzalendo ashiriki kikamilifu katika kuepusha jambo lolote ovu kwa mwenzake kwa lengo la kuendeleza ujirani mwema na pia kudumisha amani na usalama.

Kwa lengo la kutilia mkazo umuhimu wa shuhguli za ulinzi shirikishi katika mikutano yake mbali mbali Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amekuwa akipongeza jitihada zinazofanywa na vikundi vya polisi jamii katika kusimamia ulinzi na usalama wa mitaani.

Ameonesha kuridhishwa kwake na kazi inayofanywa na Jeshi la polisi nchini na kusisitiza kuwa ushirikiano wa jeshi hilo na wananchi haunabudi kudumishwa kwa lengo la kuimarisha usalama wa raia na mali zao. Aidha, amekuwa akitilia mkazo kuwa suala la ulinzi na usalama wa watu na mali zao ni jukumu la kila mmoja na siyo jukumu la Vyombo vya ulinzi na usalama pekee.



*Bomba la maji safi likiwa liko wazi baada ya watu wanaochimba mchinga kusababisha shimo kubwa katika chanzo cha naji huko Mwanyanya*

# Uharibifu wa miundombinu upigwe vita

Katika maisha ya kawaida ya kila siku, jamii huzaa misemo ya Kiswahili ikiwemo methali kutokana na uzoefu wa matukio katika maisha ya mwanadamu. Kutokana na matukio hayo, wazee hutumia hekima na maarifa yao kuasa, kuelimisha juu ya kuendeleza mwenendo mwema na kuachana na tabia mbaya zenye kwenda kinyume na maadili, silka au utamaduni wa jamii husika.

Tukumbuke kuwa katika lugha ya Kiswahili wahenga wametoa methali nyingi lakini kwa mnasaba wa maudhui haya tusisahau methali isemayo "usipoziba ufa utajenga ukuta." Usemi huu unaendana na wazo la kutaka jamii kwa jumla kuchukua hatua muafaka ya kuilinda miundo mbinu mbali mbali dhidi ya vitendo vya hujuma vinavyofanywa na watu wachache kwa manufaa yao binafsi bila ya kujali gharama kubwa iliyotumika kuimarisha miundo mbinu hiyo.

Tumeshuhudia katika maeneo mbali mbalikwambakadirisikuzinavyoendelea, ndivyo wimbi la uharibifu wa makusudi wa miundombinu hapa Zanzibar linavyoshamiri. Yapo baadhi ya matukio ambayo huripotiwa wakati maalum lakini kwa kiasi kikubwa matukio mengi miongoni mwa yanayoshuhudiwa katika siku za hivi karibuni, yanafanyika ama kutokana na miongoni mwetu kuyafumbia macho au kwa kukosa uthubutu, kukosa uzalendo wa kweli au kwa kutokujua wajibu wetu.

Ni ukweli uliowazi kwamba Serikali hutumia fedha nyingi kujenga miundo mbinu ya barabara za kisasa ili ziwe chachu ya maendeleo kwa wananchi wote wa Zanzibar. Serikali kupitia Idara ya ujenzi na Utunzaji wa barabara imekuwa ikichukua juhudi maalum kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi na utunzaji bora wa barabara hizo. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kuweka alama za barabarani katika maeneo tofauti kulingana na hali yenyewe ya barabara.

Katika hali isiyo ya kawaida, imeshuhudiwa katika baadhi ya maeneo hayo watu wamediriki kung'oa nguzo za usalama wa barabarani (sign posts) na kuchukua mabati ya alama na nguzo kwa matumizi yao binafsi. Imeshuhudiwa pia katika baadhi ya maeneo viguzo vya mtandao wa "e-government" navyo vimeshahujumiwa kwa namna mbali mbali kabla ya kazi iliyokusudiwa kuanza kufanyika kwenye maeneo yaliyokusudiwa. Hali hii inakumbusha matukio mabaya ya kuchomwa matairi kwenye maeneo kadhaa ya barabara maeneo ya mjini Unguja na kupelekea uharibifu mkubwa wa miundombinu.

Katika baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Magharibi kuna hujuma za uchimbaji wa mchanga zinazoendelea chini ya nguzo kubwa zinazopitisha umeme kutoka Fumba hadi Mtoni. Aidha, mara kadhaa kumekuwa na transfoma kama ile iliyoarifiwa katika mwezi wa Agosti mwaka huu, ambapo watu wasiojulikana walikata waya wa umeme kwenye transfoma ya maeneo ya Mwembeshauri na kusababisha kukosekana kwa huduma hiyo kwa siku kadhaa.

Tukio jengine la hivi karibuni kabisa ni jaribio la kutaka kuiba vifaa muhimu vya umeme kwenye transfoma iliyopo Vuga karibu na Kampasi ya SUZA inayogawa umeme katika hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja na maeneo kadhaa ya mji Mkongwe zikiwemo ofisi za Serikali, hoteli za kitalii na makaazi ya watu.

Jitihada za Serikali za kuimarisha miundo mbinu ya kuondoa maji machafu katika mji wa Zanzibar nazo zinakabiliwa na changamoto kubwa ya wizi wa mafuniko ya makaro ya chuma. Inaaminika kwamba vyuma hivyo vinauzwa kwa wafanyabiashara ya makachara ambao wengi wao wanajulikana. Aidha, wanunuaji wa makachara wanafahamu kwamba baadhi ya vyuma wanavyovinunua ni mali ya Serikali iliyopatikana kwa njia ya wizi.

Gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 8 Septemba 2014 limeandika taarifa ya kusikitisha kuhusiana na wizi wa nondo za uzio wa Uwanja wa michezo wa Amani mjini Unguja. Uwanja huo, ambao ulifunguliwa mwaka 1970 na Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarange Nyerere, kutokana jitihada za wananchi wa Zanzibar chini ya Mwasisi wa Mapinduzi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kutaka kuimarisha sekta ya michezo nchini, umeipa heshima kubwa Zanzibar kimichezo.

Hadi Zanzibar inatimiza miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964, Uwanja huo uliendelea kuonekana haiba yake, na hasa baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China.

Wakati umefika sasa kwa jamii kubadilika na kutoyafumbia macho maovu kama hayo yanayoendelea kufanyika katika miundombinu yote, hasa ikitiliwa maanani kwamba Serikali hutumia fedha nyingi za wananchi kwa maslahi yao na taifa kwa jumla. Ni jukumu la kila mmoja kufahamu kwamba mjenga nchi ni mwananchi mwenyewe.



*Uchimbaji wa mchanga unavyoendelea Mwanyanya umekuwa ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa miundombinu mbali mbali kama ya umeme na maji*

# Usalama na afya kazini ni kielelezo cha Utawala Bora



*Wakaguzi wa Usalama na Afya Kazini wakitoa elimu ya Usalama na Afya Kazini kwa Wafanyakazi wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) Tawi la Mpirani Zanzibar, tarehe 04 Septemba 2014*

Kuwepo kwa hali ya usalama na kuzingatiwa kwa afya za wafanyakazi katika sehemu za kazi ni miongoni mwa masuala yaliyopewa umuhimu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein.

Ni wazi kuwa kuwepo kwa mazingira salama ya kufanyia kazi yanayozingatia pia umuhimu wa kulinda afya za wafanyakazi kuna mchango mkubwa kwa kuongeza ufanisi katika maeneo ya kazi iwe maofisini, mashambani na viwandani kwa watumishi wa sekta ya umma na binafsi. Aidha, hali hii huongeza ufanisi kazini kwani



*Baadhi ya mafundi wakiwa katika kazi zao huko Shangani Mji Mkongwe wa Zanzibar bila ya kuwa na vifaa vya kinga kwa usalama na afya zao, hali hii imekuwa ikihatarisha maisha ya wafanyakazi*

huwachochea watumishi kuhisi kuwa wanathaminiwa na waajiri wao.

Kwa kutambua umuhimu huo Serikali ya Mapinduzi Awamu ya saba ilianzisha Idara ya Usalama na Afya Kazini, chini ya Kamisheni ya Kazi katika Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma ili kuratibu na kusimamia masuala hayo. Kuwepo kwa Idara hii ni kutimiza matakwa ya kisheria chini ya kifungu nambari 4 cha sheria ya Usalama na Afya Kazini, nambari 8 ya mwaka 2005.

Lengo la msingi la kuanzishwa kwa idara hii ni kuweka masharti bora ya usalama, afya na ustawi wa wafanyakazi na kuwalinda watu wengine dhidi ya hatari kwa usalama na afya zinazotokana na zinazohusiana na shuhguli za kazi.

Ili kutekeleza lengo la kuanzishwa kwa Idara hii kwa mujibu wa sheria ya Usalama na Afya Kazini, Idara hii inatekeleza majukumu kadhaa yakiwemo kufanya ukaguzi katika sehemu zote za kazi iwe rasmi au zisizo rasmi isipokuwa zile zinazotolewa msamaha na waziri anayehusika na masuala ya kazi kwa mujibu wa sheria. Jukumu jengine ni kuandaa kanuni na miongozo ya Usalama na Afya kazini kutokana na sheria iliyopo na kuwepo kumbukumbu za viwango vya usalama na afya vya Kitaifa na Kimataifa.

Majukumu mengine ya Idara ni pamoja na kuhakikisha ujenzi wa majengo yanayotumikia kwa kazi yamebuniwa na kujengwa vizuri kwa ajili ya kuwalinda wafanyakazi na watumiaji wengine wasidhurike . Kuratibu na kuandaa miongozo ya uchunguzi wa afya za wafanyakazi kadhalika kusimamia na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanafanyiwa uchunguzi wa afya zao kabla na baada ya kuajiriwa na wanapoacha au kuachishwa kazi au inapotokea dharura yoyote.

Mfanikio makubwa yamepatikana tokea kuanzishwa kwa Idara hii mwaka 2011 chini ya Serikali ya Dk. Ali Mohamed Shein. Akizungumza na jarida la Ikulu Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Afya kazini Ndugu Suleiman Khamis Ali ameyataja mafanikio yaliyopatikana kuwa ni pamoja kuongezeka kwa uelewa wa suala la usalama na afya kazini kwa baadhi ya waajiri na wafanyakazi kwenye sehemu za kazi kutokana na elimu inayotolewa na Idara hiyo wakati wa ukaguzi na kupitia vipindi vya redio, televisheni na vipeperushi vinavyosambazwa. Hivi sasa Sera ya Usalama na Afya kazi na mpango wa miaka mitano(5) wa utekelezaji vimo katika hatua za mwisho ambavyo vitarahisisha utekelezaji bora wa shuhguli za usalama na afya katika sehemu zote za kazi hapa nchini.

Mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa mfumo wa kuweka wawakilishi wa masuala ya Usalama na Afya kazini katika kila wizara na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Unguja na Pemba ili kuweza kutekeleza kwa ufanisi sheria hii. Kuanzisha daftari la Usajili kwa ajili ya kuzisajili taasisi za kazi nchini kwa lengo la kurahisisha shuhguli za ukaguzi kwa kutambua mazingira ya kazi zao na hatari zinazoweza kutokea na kutoa ushauri unaofaa. Zaidi ya hayo kuna mafanikio makubwa ya kuimarika kwa mashirikiano baina ya Idara hii na taasisi za serikali na binafsi katika kuhakikisha kuwepo kwa mazingira bora ya usalama na afya katika sehemu za kazi.

Bila ya Shaka, utekelezaji mzuri wa majukumu ya Idara hii na kupewa ushirikiano na taasisi zote ndiko kutakakopelekea kufanikisha azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba na utekelezaji wa dhana ya utawala bora.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitoa hotuba yake mbele ya wananchi na wafanyakazi wa Kituo cha Kukaushia Embe katika kijiji cha Cheju Kibonde maji Wilaya ya Kati Unguja wakati alipokizindua Kituo hicho, tarehe 24 Julai 2014*

# Wananchi wa Cheju wanavyoshuhudia mabadiliko ya hali zao za maisha

Wataalamu wa uchumi, mawasiliano na habari duniani kwa muda mwingi wamekuwa wakisumbuka kutafuta lugha nyepesi itakayowawezesha wananchi hasa vijijini kufahamu kwa urahisi maana ya maneno ya kitaalamu yanayotumika katika nyanja na sekta tofauti kama vile uchumi, ufundi, utamaduni na nyengine nyingi.

Ugumu wa kazi hiyo unatokana na kasi kubwa ya maendeleo duniani ambayo inakwenda sambamba na ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Misamiati mingi ambayo imekuwa ikiibuliwa ndani ya lugha ya Kiswahili inachelewa kufahamika miongoni mwa waswahili wenyewe.

Maneno kama vile ukuaji wa uchumi au pato la taifa ni maneno maarufu miongoni mwa wataalamu wa masuala ya uchumi lakini siyo wengi vijijini wenye kufahamu maana halisi ya maneno hayo. Utata wa maneno hayo huongezeka zaidi pale hali zao za maisha zinapoonekana kuwa bado ziko duni.

Kwa kuwa mantiki yenyewe ya ukuaji wa uchumi inajumuisha mambo mengi, jitihada maalum zimekuwa zikichukuliwa kuwaelimisha wananchi maana ya kukua uchumi na namna watu wa kawaida wanavyonufaika kutokana na ukuaji huo.

Hata hivyo, imedhihirika wazi kwamba ushahidi wa vitendo au picha halisi ya jambo husika ndio njia pekee inayowawezesha watu wengi kufahamu maana ya jambo linalokusudiwa kwa urahisi.

Wananchi wa kijiji cha Cheju katika Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja wameelezea jinsi walivyoifahamu vyema maana ya kukua kwa uchumi Zanzibar, kutokana na mabadiliko makubwa ya hali zao za maisha ya sasa wakilinganisha na kipindi kifupi cha miaka mitatu iliyopita.

Wananchi hao wamekuwa wawazi kubainisha mafanikio wanayoyaona kiuchumi na kijamii ambayo wameyashuhudia ndani ya kipindi kisichozidi miaka mitatu na matarajio makubwa ya hali bora zaidi za maisha waliyonayo katika kipindi kijacho.

Bibi Hamida Mahamoud Mzee mkaazi wa kijiji hicho ameielezea Cheju ya leo kuwa ni kijiji cha maendeleo kutokana na wananchi kufaidika na huduma muhimu za kiuchumi na kijamii kama vile barabara, maji safi na salama, huduma za umeme, elimu na afya.

Jitihada za Serikali za kuimarisha uchumi na kuinua hali za maisha ya wananchi, zimebadilisha ufahamu wa wananchi kuhusiana na kijiji hicho ambacho, kimsingi kilifahamika kutokana na umaarufu wa shughuli za kilimo cha mpunga pekee.

"Zamani ilikuwa ukikitaja kijiji chetu ilikuwa inakujia picha ya kilimo cha mpunga mabondeni, lakini Cheju ya sasa ni zaidi kuliko kilimo cha mpunga kutokana na juhudi kubwa za kukuza uchumi na pato la mwananchi zinazochukuliwa na Serikali." Alisema Bibi Hamida.

Hata hivyo Bi Hamida ametoa wito kwa wananchi wa Cheju kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuunga mkono juhudi hizo kwani alisema, bila ya Serikali kuungwa mkono maendeleo hayo hayawezi kuwafikia kwa haraka.

Bw. Juma Mabuba Kuyela mkaazi wa Cheju amesifu utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Rais wa Zanzibar na



*Baadhi ya wafanyakazi na watu waliohudhuria uzinduzi wa Kituo cha Kukaushia Embe katika kijiji cha Cheju Kibonde maji Wilaya ya Kati Unguja wakimsikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitoa hutoba wakati wa uzinduzi wa kituo hicho, tarehe 20 Agosti 2014*

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika maeneo tofauti, jambo ambalo amesema ni tofauti na wanasiasa wengi hapa nchini.

Alisema miradi iliyokwishatekelezwa na ile inayoendelea kutekelezwa kama vile mradi wa ujenzi wa barabara, skuli ya msingi, chekechea iliyojengwa kwa msaada wa Serikali ya Korea kupitia mpango unaojulikana SEAMAUL UDONG kwa kushirikiana na taasisi za Serikali ya Mapinduzi, imekuwa mkombozi mkubwa kwa watoto wa kijiji cha Cheju na maeneo ya jirani ambao ndio tegemeo kubwa la taifa la kesho.

"Miradi hiyo ambayo ni utekelezaji wa ahadi za Rais imelenga kuwakomboa wananchi kutoka katika dimbwi la umasikini" alisema.

Bwana Mabuba ameongeza kuwa mbali na miradi hiyo, kijiji cha Cheju kimepata mwelekeo wa kujinasua kutoka katika tatizo sugu la umasikini kutokana na mradi wa kiwanda cha kusindika embe hatua ambayo itawasiadia wananchi wa Cheju kupata soko la uhakika la kuuza embe kwenye kiwanda hicho, na pia soko la bidhaa zitakazozalishwa kiwandani hapo, kwani alisema embe ni zao linalopatikana kwa wingi katika kijiji hicho na kwa muda mrefu zimekuwa zikitupwa ovyo wakati msimu unapofika.

"Wakati wa msimu wa embe Cheju inakuwa na embe nyingi sana ambazo hupotea ovyo kutokana na kukosa sehemu na taaluma ya kuzihifadhi, lakini kuwepo kwa kiwanda hicho kutaweza kuwasaidia wananchi kwani watakuwa na uhakika wa sehemu ya kuuza embe zao kwa wakati unaostahiki" alisema Bwana Mabuba.

Naye Kaimu Sheha wa Shehia ya Cheju Bwana Maulid Haji Masoud amesema wananchi wa Cheju sasa wako furahani kutokana na kazi inayoendelea ya ujenzi wa barabara ambayo ilikuwa kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa kijiji hicho.

"Cheju ni sehemu yenye kutoa mazao mengi likiwemo zao la mpunga, lakini kwa kipindi kirefu wananchi walikuwa na kilio cha ukosefu wa barabara, hivyo kujengwa kwa barabara ya Jendele-Cheju-Kaebona kutabadilisha kabisa mazingira ya kijiji pamoja na hali za maisha ya wananchi wake". Alisema Kaimu sheha huyo.

Wamepongeza hatua ya Serikali ya kupunguza bei ya pembejeo za kilimo ambayo wamesema imewasaidia wakulima waliowengi ingawa kumekuwa na changamoto katika upatikanaji wa huduma hizo kwa wakati hasa matrekta pamoja na mbolea.

Mzee Mohd Ahmada Mdunga amesema wananchi wa cheju wana kila sababu ya kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa ya awamu ya saba chini ya uongozi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuwa chachu ya kuimarisha maendeleo ya kijiji cha Cheju .

Pamoja na mafanikio hayo, wananchi wa Cheju vile vile hawakusita kuzungumzia changamoto zinazowakabili katika harakati zao za maendeleo. Miongoni mwa changamoto hizo ni upatikanaji wa maji safi na salama jambo ambalo limekuwa likileta usumbufu mkubwa kwao na wameiomba Serikali kuendelea na juhudi zake za kuharakisha upatikanaji wa huduma hiyo muhimu kwani maji ndiyo uhai na maendeleo.

Wananchi wa Cheju walitoa maelezo hayo katika nyakati tofauti, siku chache baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kufanya ziara ya kutembelea kijiji chao kuona kiwanda cha kukaushia embe na kuzindua skuli ya Maandalizi ya kijiji hicho inayoendeshwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Korea na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katika nasaha zake Dk. Shein amewataka wananchi wa kijiji cha Cheju kuchangamkia maendeleo kwa kuongeza nguvu na jitihada zao ili kuwapa moyo wafadhili wanaosaidia miradi ya maendeleo nchini.

Kuhusu utekelezaji wa ahadi mbalimbali kwa wananchi wa Cheju, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alisema ahadi zote alizowaahidi katika vipindi mbali mbali zimeanza kutekelezwa ikiwemo ujenzi wa barabara ya Jendele kupitia Cheju hadi Unguja Ukuu Kaebona kwa kiwango cha lami.

Kuhusu tatizo la maji safi na salama, Dk. Shein aliwaeleza wananchi hao kuwa ahadi hiyo imeanza kutekelezwa chini ya mpango wa kuipatia Wilaya ya Kati maji safi na salama, ambapo hivi sasa kazi za ujenzi wa miundombinu zinaendelea kufanyika katika maeneo mbali mbali Wilayani humo.




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwa na Mkuu wa Kitivo cha Tiba DEAN Ulpiano Perez kutoka Cuba pamoja Waziri wa Afya Rashid Seif Suleiman wakiwa katika Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya wakati wa Mahfali ya kwanza yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo Mbweni nje ya Mji wa Unguja, tarehe 28 septemba 2014*